# Nipashe

Jumanne Mei 28, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581690

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**MBAPPE: NITATANGAZA WAPI NAENDA**

UKURASA 22

**WAHOJIWA** na polisi undani anayedaiwa kuuawa na mkewe

UKURASA 3

**VIGOGO** h'shauri, mifuko ya hifadhi waongoza tuhuma za ufujaji wa mali

UKURASA 4



**LAINI** 17,000 za 'tuma kwa namba hii' zafungwa

UKURASA 5

## YALIYOMO

UKURASA WA 17

**TATHMINI ONGEZEKO LA WAGUMBA ZANZIBAR HAIJAFANYIKA**

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema hadi sasa haijafanya tathmini ya kina...

UKURASA WA 17

**'HAKUNA UTAFITI WA ONGEZEKO LA RUSHWA, UHUJUMU UCHUMI'**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman amesema...

UKURASA WA 17

**VIJANA WAJUZI WA TEHAMA WANAHITAJIKA ZANZIBAR**

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni...

**Wajukuu watoa ushahidi kortini bibi kuunguza makalio yao**

UKURASA 3

# Kauli ya Makonda yapingwa vikali



**PROFESA,** wanaharakati wataka ajitathmini...

Ukurasa wa 2&9

Makonda — Chatanda — Dk. Nkya — Prof. Chisanga



## Hoja ya Askofu Shoo rushwa ya aibu yawaibua wadau uchaguzi

**Na Christina Mwakangale**

KAULI ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Dk. Fredirick Shoo juu ya "rushwa ya aibu katika uchaguzi" imeibua wadau wa siasa, wakitaka Watanzania wawe kitu kimoja kuchagua viongozi wenye maadili na si wanaotumia fedha chafu.

Juzi Askofu Dk. Shoo alitaja ubinafsi kuwa ni sumu mbaya iliyofikisha baadhi ya watu kwenye hatua ya kutaka fedha chafu ili kupata madaraka kwa lengo la kujinufaisha wao na familia zao badala ya maslahi...

Endelea Uk. 2

**MICHEZO** AUCHO ATAMANI KUCHEZA NA CHAMA UK 24

MAONI, KATUNI UK.6



Wageni mbalimbali waliotembelea Maadhimisho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu wakipata maelezo katika banda la maonyesho la Chuo Kikuu Mzumbe jana viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal jijini Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hoja ya Makonda yapingwa vikali

**Na Restuta James**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amewajibu waliomwonya kutoa kauli wanazodai zinadhalilisha watumishi wa umma.

Amesema hatishwi na kauli zao na ni kama wanambembeleza na kumwongezea nguvu ya kufanya kazi.

Majibu hayo yamekosolewa vikali na baadhi ya viongozi na wadau wa siasa, wakimtaka ajitathmini kiutendaji.

Mei 24 mwaka huu, ilisambaa video fupi ikimwonesha Makonda akimhoji mtumishi mwanamke wilayani Longido, wakosoaji wakidai mkuu wa mkoa huyo alitumia lugha ya udhalilishaji dhidi ya mtumishi huyo.

Baada ya kusambaa kwa video hiyo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT), walimwonya Makonda dhidi ya madai hayo ya udhalilishaji wanawake na watumishi wa umma.

Jana ikiwa ni muda mfupi baada ya Makonda kuwajibu wanaomkosoa, Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba (JUKATA), Dk. Ananilea Nkya, alikosoa kauli ya Makonda, akisema kiongozi makini hadhalilishi wenzake bali anazingatia miiko, kanuni na taratibu za uongozi.

“Uongozi bora ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya taifa na kiongozi bora yeyote hatafuti umaarufu kwa kudhalilisha wengine, kiongozi bora anazingatia maadili, anaonya na kufuata misingi ya kazi. Hawezi kuongea maneno ya chumbani hadharani,” alisema.

Dk. Ananilea alidai maneno ya Makonda kwa baadhi ya watumishi mkoani Arusha yanatweza utu wa wanaume na wanawake na hata yeye (Makonda), asingependa mke wake atolewe maneno makali mbele ya watu.

“Kiongozi bora siyo yule anayedhalilisha wenzake mbele ya wananchi kutafuta umaarufu, kiongozi bora anafuata misingi ya uongozi. Akumbuke kwamba yeye ni mwakilishi wa Rais, anapaswa kulinda haiba ya kiongozi aliyemteua,” alisema.

Profesa Askofu Victor Chisanga (mstaafu wa Chuo Kikuu cha Ardhi) alidai utendaji wa Makonda unadhihirisha namna CCM imeshindwa kuhudumia wananchi.



Msomi huyo ambaye kwa sasa ni Askofu wa Kanisa la World United Alliance Church in Tanzania (WUAC-Tanzania), alisema: “Mungu aliniambia kwamba kazi ya Makonda ni nzuri na mbaya. Ni nzuri kwa sababu inaweka wazi kuharibika na kushindwa kazi kwa CCM na serikali yake na ni mbaya kwa sababu anaipa ‘oyee’ izidi kukaa madarakani wakati ni wazi haifai tena.”

Mwenyekiti wa UWT, Mary Chatanda, alipotafutwa na Nipashe jana, alikataa kuzungumzia kauli mpya ya Makonda dhidi ya “wanaopiga kelele” kwa madai kuwa hajaisikia.

“Sijui chochote, nilikuwa kwenye kazi zangu, subiri niangalie taarifa ya habari nione alichosema,” alisema Mary.

Wiki iliyopita Mary alisema, “Nimesikitishwa sana na hawa viongozi mnaowateua, kunyanyasa na kudhalilisha watendaji wanawake kwenye sehemu zao za kazi.

“Nimesikitishwa sana na kipande cha video kilichozunguka kule Longido, haikuwa jambo jema, si jambo zuri hata kidogo, kama wewe ni kiongozi mkubwa wa serikali unamwona mtendaji wako wa chini amekosea, huwezi kuwa na kauli na ulimi usio mzuri.

“Ni vizuri ukakaa nao ukazungumza nao, una nafasi ya kumwita na kumwambia kwa masuala ya udhalilishaji wanawake Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti hatutakubaliana nayo, haiwezekani, tunaomba tuheshimiwe wanawake, tena sisi ni watendaji wazuri kuliko hao wanaume.”

**SOMA TAARIFA ZAIDI Uk. 9**

## Kauli ya Askofu Shoo rushwa ya aibu yaibua wadau uchaguzi

**Na Christina Mwakangale**

KAULI ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Dk. Fredirick Shoo juu ya “rushwa ya aibu katika uchaguzi” imeibua wadau wa siasa, wakitaka Watanzania wawe kitu kimoja kuchagua viongozi wenye maadili na si wanaotumia fedha chafu.

Juzi Askofu Dk. Shoo alitaja ubinafsi kuwa ni sumu mbaya iliyofikisha baadhi ya watu kwenye hatua ya kutaka fedha chafu ili kupata madaraka kwa lengo la kujinufaisha wao na familia zao badala ya maslahi ya taifa.

Katika mazungumzo na Nipashe kuhusu kauli hiyo jana; Mchambuzi wa Siasa, Abbas Mwalimu, alisema alichokisema Askofu Shoo si jambo geni, linahusiana na maadili, hasa wakati wa uchaguzi.

“Kinachotokea ni kwamba ukichagua kiongozi ambaye ametumia fedha zake, maana yake ni kwamba atakapopata uongozi atahitaji kurudisha fedha yake, sasa zinarudi vipi? Ndio Askofu Shoo, anakieleza.

“Hatuna kiongozi ambaye tunaweza kumwajibisha, tutakuwa na kiongozi ambaye anaweza kujiwajibikia mwenyewe, kwa sababu tayari ameshatulipa kwenye kura, ni kama ukienda dukani ukanunua bidhaa, mkate na ukishaununua unabaki kuwa wako, ameshawanunua watu kama bidhaa,” alisema Abbas.

Alisema kuwa alichokisema Askofu Dk. Shoo kinaakisi na Katiba, Ibara ya 8(1)(a) inaelekeza “wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba”.

Pia alirejea kifungu cha 1(b) na (c) vya ibara hiyo ya Katiba kinachoeleleza kuwa lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi na serikali itawajibika kwa wananchi.

“Abbas alisema, “anachosema Askofu Shoo ni kwamba tuchague viongozi ambao tunaweza kuwawajibisha. Wakati wa kampeni ulituambia utatekeleza a, b, c, atuambie ametekeleza nini ndani ya miaka miwili?

“Wabunge wanaweza kumwajibisha Rais, wana uwezo kumwajibisha waziri mkuu kwa mujibu wa Katiba, pia wana uwezo kumwajibisha makamu wa rais, spika, jiulize nani anamwajibisha mbunge mwenyewe? Ni mwananchi.

“Inatakiwa mwananchi amhoji mbunge wake, mbali na ilani ya chama cha siasa, kuna ilani ya mbunge, mwananchi amwulize mbunge wake, askofu anamaanisha kama kura zinanunuliwa kwa rushwa, ni vigumu kumwajibisha kiongozi aliyechaguliwa na ameingia katika uongozi kwa rushwa,” alisema Abbas.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba (JUKATA), Dk. Ananilea Nkya, alisema anaunga mkono hoja ya Askofu Dk. Shoo, kwamba kiongozi anayepatikana kinyume cha maadili hafai kuongoza umma.

“Kiongozi wa aina hii akipata uongozi atahakikisha anatumia rasilimali za umma kurejesha fedha zake. Atakuwa mtu ambaye hana sifa ya uongozi, kwa sababu atakuwa amenunua uongozi.

“Uongozi bora ndio rasilimali namba moja ya maendeleo ya taifa lolote, maana yake mtu wa ovyo hana sifa za uongozi. Kiongozi bora ana ubunifu, mwajibikaji, akiona ametoa fedha yake yeye hana shida anawaza kutafuta fedha kubwa ili aje ahonge zaidi,” alisema Dk. Ananilea.

Alisema kwamba wakati nchi inaingia katika mfumo wa vyama vingi, lengo lilikuwa kuboresha maisha, ingawa hadi sasa mfumo huo haujatimiza malengo hayo kutokana na baadhi ya viongozi kufanya anachokilalamikia Dk. Shoo.

“Wakati umefika sasa Watanzania tuamke. Kuna wanafunzi wanamaliza vyuo, hawana kazi, tuna rasilimali kibao. Askofu Shoo tunamwunga mkono kiongozi huyu wa kidini, mtu hata kama anawania uenyekiti, ubunge, udiwani, urais asipewe kama hana sifa,” alihimiza Ananilea.

Mkazi wa Ukonga, jijini Dar es Salaam, Daudi Amos, akitoa maoni yake, alisema wananchi wanapenda kuwa na kiongozi ambaye anakuja kutatua changamoto zao ingawa baadhi ya matarajio hayo hayafanikiwi.

“Kiongozi ambaye mimi ninamhitaji ni yule ambaye ana jicho la kutukomboa, tena kwa masuala madogo tu mtaani. Kiongozi akiomba kura anashinda, akishapata uongozi hamwoni. Au unamchagua kiongozi huyu, analetwa mwingine, uchaguzi nao ni kama pata potea tu,” alisema Daudi.

Juzi, Askofu Dk. Shoo alitoa wito kwa wanaoipenda nchi yao kuwa sauti moja kuhakikisha viongozi waliopo kwenye madaraka na mamlaka wawajibike kwa ajili ya ustawi wa taifa.

Alionya kuwa ndani ya vyama vya siasa kuna migongano mikubwa kiasi kwamba wengi hawajui mwelekeo ni wapi, shida kubwa akitaja ni ubinafsi; kila mtu anaangalia mambo yake na si ustawi wa kundi, nchi na vizazi vyake.

HABARI KITAIFA

# Wajukuu watoa ushahidi kortini bibi yao kuwaunguza makalio

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imeanza kusikiliza kesi inayomkabili mkazi wa Mtaa wa Kagera mjini hapa, Anasitazia Maziku (62), anayeshtakiwa kuwachoma moto wajukuu zake wawili.

Mshtakiwa huyo anadaiwa kuwachoma moto kwenye makalio na kuwasababishia majeraha na maumivu, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Nyakato Bigirwa na aliposomewa mashtaka yake alikana kuhusika na makosa hayo na yuko nje kwa dhamana ya wadhamini wawili na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tatu kwa kila mdhamini.

Upande wa mashtaka unaongozwa na Mawakili wa Serikali, Mussa Mlawa na Deodatha Dotto, ambao walidai mahakamani wana mashahidi wawili ambao ni waathirika wa tukio hilo na wako tayari kuwasikiliza.

Hakimu Bigirwa alimwuliza mshtakiwa kama yuko tayari kuwasilikiza mashahidi wawili wa upande wa Jamhuri, naye akajibu yuko tayari.

Baada ya mshtakiwa huyo kudai yuko tayari, Hakimu Bigirwa alimwambia Wakili wa Serikali Deodatha Dotto aendelee.

Shahidi wa kwanza na wa pili; wa kwanza ni mvulana (10) na wa pili ni msichana (7), walidai mahakamani kuwa siku ya tukio hilo, Septemba 22, 2023, mshtakiwa ambaye ni bibi yao aliwatuma wanafunzi hao wa Shule ya Msingi Nyanza kwenda dukani kuchukua betri ya simu.

Shahidi wa kwanza alidai kuwa kutokana na kuchelewa kurejea nyumbani, bibi yao aliwafuata, njiani walipomwona walikimbia hadi nyumbani.

Alidai kuwa bibi yao alipofika nyumbani aliwakamata na kuwafunga kamba mikononi na miguuni kisha kuwacharaza fimbo na baadaye alichukua kiwashio cha randa za mbao na kuwachoma moto kwenye makalio kisha kuwafungua kamba na kuwapa kazi za kufanya.

Alidai kuwa yeye alipewa kazi ya kulima shambani na mdogo wake alipewa kazi ya kuosha vyombo. Baadaye walitoa taarifa kwa baba yao, Shukrani Jumapili ambaye alikwenda Kituo cha Polisi Geita na kufungua shauri kisha kuwapeleka watoto wake wote wawili katika Hospitali ya Mkoa wa Geita kwa ajili ya matibabu.

Baada ya shahidi wa kwanza wa upande wa Jamhuri kumaliza kutoa ushahidi wake, Hakimu Bigirwa alimwuliza mshtakiwa kama ana maswali ya kumuuza shahidi wa upande wa Jamhuri. Naye alidai anayo na kumwuliza shahidi kama kweli alimfunga kamba, kumchoma moto, shahidi huyo akidai kutendwa mambo hayo na mshtakiwa.

Baada ya mshtakiwa huyo kumaliza kumwuliza maswali shahidi wa upande wa Jamhuri, Wakili wa Serikali Dotto aliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine waliobakia.

Hakimu Bigirwa alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Juni 10 mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi waliobakia.

## Wahojiwa na polisi undani wa anayedaiwa kuuawa na mkewe

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WATU kadhaa wanahojiwa akiwamo mwanamke anayedaiwa kuwa chanzo cha mgogoro uliosababisha mauaji ya mfanyabiashara wa Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, Evagro Msele.

Mfanyabiashara huyo (43) anadaiwa kuuawa na mkewe, Beatrice Elias (36), mkazi wa Mtaa wa Katanini, Wilaya ya Moshi saa tatu usiku wa Mei 25 mwaka huu huko katika Kitongoji cha Pumuani A, Kata ya Kirua Vunjo baada ya kumkuta kwa mzazi mwenzake.

Wakati mwanamke huyo (jina limehifadhiwa) akiendelea kuhojiwa na Jeshi la Polisi kuhusiana na tukio hilo, Nipashe jana ilifika nyumbani kwa Msele ulikowekwa msiba, ilishuhudia babu wa marehemu (jina tunalo), akielekeza watoto sita wa marehemu wajiandae kwenda kumwona mama yao mahabusu.

Jana, Philip Msele, mjomba wa marehemu wakati anatoa taarifa ya familia kwa waombolezaji, alisema mwanamke anayehojiwa alikuwa amezaa na marehemu mtoto mmoja mwenye umri wa miaka saba.

Philip alisema tayari polisi wamekabidhi mwili wa ndugu yao kwa familia kwa ajili ya kuendelea na taratibu za mazishi.

"Leo (jana) tulikwenda pale Kituo Kikuu cha Polisi Moshi saa mbili asubuhi na tukaelekezwa kwenda pale KCMC (Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini) na uchunguzi umefanyika chini ya madaktari, polisi na familia.

"Ni kweli Evagro Michael Msele ana watoto saba, sita kwa mke wa ndoa (Beatrice) na huyo mwingine, ana mtoto naye mmoja mwenye umri wa miaka saba. Msele atazikwa nyumbani kwake Mtaa wa Katanini, Kata ya Msaranga, Manispaa ya Moshi," alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, mke wa ndoa Beatrice, alimvizia mumewe akitoka nyumbani kwa mzazi mwenzake na kumchoma na kitu chenye ncha kali.

Juzi Kamanda Maigwa alisema wanamshikilia Beatrice kwa mahojiano zaidi.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

## Kaya 1,373 zahama kwa hiyari NCAA tangu 2022

**Na Jenifer Gilla**

JUMLA ya kaya 1,373 zenye watu 8,364 zimekubali kuhama kwa hiyari katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) tangu mpango wa kuwahamisha kwa hiari ulipoanza Juni 2022.

Serikali imesema mpango wa kuwahamisha kwa hiyari kupitia elimu na uhamasishaji unaendelea ili kufikia idadi yote ya wakazi takribani 198,000 wanaotarajiwa kuhama kwenda katika vijiji vya Msomera wilayani Handeni, Saunyi wilaya ya Kilindi na Kitai, Simanjiro.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhage Matinyi, alisema uhamishaji huo unasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia NCAA.

Alisema tangu mpango huo ulipoanza Juni, 2022, jumla ya kaya 1,373 zenye watu 8,364 zimeshahama, kaya 1,248 zenye watu 7,547 zikienda Kijiji cha Msomera na kaya 125 zenye watu 817 katika vijiji vya Saunyi na Kitai.

Alisema uhamaji huo pia ulihusisha jumla ya mifugo 36,457 ambapo 30,314 ilikwenda Msomera na 6,143 ikielekea kwenye maeneo mengine.

Ili kufanikisha mpango huo, serikali na NCAA ziliweka mkakati wa maalum wa uelimishaji, uhamasishaji na uandikishaji ukijumuisha timu ya viongozi na watendaji wa serikali za mitaa ndani ya NCAA.

Alisema timu hiyo kwa kushirikiana na wataalamu wa ustawi wa jamii imeshawafikia wananchi wengi wanaohusika na uhamaji hiari kupitia nyumba za ibada, minada, mikutano ya hadhara, viongozi wa kimila, watu maarufu na wenyeviti wa vitongoji na vijiji.

Matinyi alisema mkakati huo unafuata maeneo yaliyogawanywa katika kanda tano za kaskazini, kusini, mashariki, magharibi na kati mwa Tarafa ya Ngorongoro ili kuhakikisha kata zote 11, vijiji vyake na vitongoji zinafikiwa.

Alisema mpango wa serikali ni kujenga nyumba 5,000 kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ambapo 2,500 zitajengwa katika Kijiji cha Msomera, Kitwai nyumba 1,500 na Saunyi nyumba 1,000.

Alisema katika Kijiji cha Msomera nyumba 1,000 zimeshakamilika, 737 zimeshakabidhiwa kwa wananchi na 263 zilizobakia ziko tayari kwa ajili ya kupokea kaya ambazo muda wowote kuanzia wiki ijayo zitapelekwa.

"Nyumba nyingine 1,500 bado ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi ili kufikisha idadi ya nyumba iliyokusudiwa," alisema Matinyi.

Alisema pia nyumba nyingine 2,500 zinatarajiwa kujengwa katika eneo la Kitwai na Sauni na upimaji wa viwanja umeshafanyika.

Matinyi alisema hifadhi hiyo imeendelea kupokea idadi kubwa ya wageni ambapo kati ya Julai 2023 na Aprili 2024, ilifikia watalii 780,281.

Alisema kupitia ugeni huo yamepatikana mapato ya Sh. bilioni 188.5 na kuvuka lengo la Sh. bilioni 155.4, akitamba ni matunda yaliyotokana na filamu ya The Royal Tour.

# Wakurugenzi, mifuko hifadhi ya jamii walalamikiwa ufujaji mali

**Na Joseph Mwendapole**

RIPOTI ya Sekretarieti ya Maadili kwa Viongozi wa Umma imeonesha wakurugenzi wa halmashauri za wilaya, manispaa, miji na majiji wanaongoza kwa kulalamikiwa kutumia vibaya madaraka na rasilimali za umma.

Iliwasilishwa mwishoni mwa wiki kwa wahariri wa vyombo vya habari na Kamishna wa tume hiyo, Jaji mstaafu Sivangilwa Mwangesi, ikionesha kundi hilo linafuatwa na kundi la watendaji wakuu wa taasisi na mameneja.

Alisema kuna ongezeko la malalamiko ya watendaji wakuu wa taasisi na mameneja kwa asilimia 100 kutokana na ucheleweshaji utoaji huduma kwa wakati hasa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Mathalani, katika kipindi cha miaka miwili iliyopita wastani wa uwasilishaji malalamiko kwa mwezi uliongezeka kutoka malalamiko 16 mwaka 2021/22 hadi malalamiko 18 kwa mwaka wa 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 13 na ongezeko hili la malalamiko limesababishwa na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi baada ya kupata elimu," alisema.

Jaji mstaafu Mwangesi alisema kulinganisha malalamiko yaliyotolewa kwa mihimili mitatu, bado taasisi zilizo chini ya serikali zinaongoza kwa kulalamikiwa zaidi zikifuatwa na mahakama na Bunge.

Kuhusu wizara, alisema Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), hasa viongozi walioko katika mamlaka za serikali za mitaa (halmashauri) inaongoza kwa kulalamikiwa zaidi na wananchi.

"Katika mwaka wa 2022/23 viongozi walioko TAMISEMI bila kujali kuwa wanawajibika kwa Sheria ya Maadili, viongozi wanaolalamikiwa waliongezeka kwa asilimia 19 kulinganishwa na mwaka 2021/22, kimsingi bado TAMISEMI imeendelea kuwa na malalamiko mengi," alisema.

Jaji mstaafu Mwangesi alisema kuwa kwa mwaka 2021/22, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kulikuwa na malalamiko 63, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (7), mahakama (5), Wizara yenye dhamana ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana (6), Wizara ya Mambo ya Ndani (12) na Wizara ya Fedha (10).

Alibainisha kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ilikuwa na malalamiko manne (4), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (4), Wizara ya Afya (3) na Bunge (6), hivyo kuwa na jumla ya malalamiko 120.

Alisema kwa mwaka 2022/23, TAMISEMI kulikuwa na malalamiko (93), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (16), mahakama (15), Wizara ya Mambo ya Ndani (15) na Wizara ya Fedha (11).

Alisema Wizara yenye dhamana ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ilikuwa na malalamiko manane (8), Wizara ya Afya (8), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (7), Wizara ya Maliasili na Utalii (4) na Bunge (2), hivyo kuwa na jumla ya malalamiko 179.




Vyombo vya moto vikipita kwa shida na kukwama kutokana na ubovu wa barabara ya Goba Tegeta A, eneo la kwa Ndosi jijini Dar as Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Kinana apigia debe kampeni ya Samia nishati safi kupikia

**Na Maulid Mmbaga,** NGERENGERE

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulurhaman Kinana, amesema kampeni ya nishati safi ya kupikia iliyoanzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inalenga kumtua mwanamke mzigo wa kuni kichwani na kumpa muda mwingi wa kujikita katika shughuli za maendeleo.

Akizungumza na wanachama wa CCM Kata ya Ngerengere, Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki jana, Kinana alisema uamuzi huo wa Rais Samia unakusudia kusaidia kuinua wanawake.

Mbunge wa jimbo hilo, Hamisi Taletale alitumia mkutano huo kuwasilisha taarifa ya utekelezaji Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 na kushirikiana na kampuni ya Oryx kukabidhi mitungi ya gesi 800 kwa wananchi kwa ajili ya kupikia.

Kinana alisema kuwapo nishati safi kwa ajili ya kupikia ni matokeo ya sera na ubunifu wa Rais Samia ambaye mwaka jana alianzisha mchakato wa kuwatua kinamama mzigo wa kuni kichwani sambamba na kuanzisha mradi wa nishati safi na salama ya kupikia.

"Pia lilifanyika kongamano kubwa, Rais akaona kwamba shughuli hii inahitaji fedha nyingi sana, kuungwa mkono na dunia nzima na msaada wa watu wenye uwezo, uongozi wake umedhihirisha yeye ni mtu wa vitendo, mbunifu, anajituma, anajitolea na mwenye kutumia maarifa katika utekelezaji mambo," alisema Kinana.

Aliongeza kuwa hivi karibuni Rais Samia alikuwa Ufaransa katika mkutano wa nishati safi ambao alikuwa mwenyekiti mwenza, mkutano ukilenga kusaidia kumtua mama mzigo wa kuni kichwani kwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi.

"Kuna maelfu ya kinamama wanafariki dunia kutokana na matumizi ya kuni na mkaa, karibu watu 50,000 wanafariki kila mwaka kutokana na kutumia nishati isiyo salama kupikia.

"Rais Samia ameamua kuanza kampeni ya kuhakikisha kila nyumba inatumia gesi ya kupika. Nchi yetu ina umri wa miaka 60, jambo hili halijawahi kufikiriwa wala kubuniwa.

"Rais Samia ameona umuhimu wake, inawezekana anawajali sana Watanzania. Ni ukweli usiopingika anawajali sana kinamama, ndio maana amelichukulia kwa uzito jambo hili.

"Sote ni mashahidi Rais alianza na kampeni kubwa ya kumtua mama ndoo kichwani na ameanza miradi mikubwa ya maji nchi nzima na miradi hii inafanyika kwa ufanisi mkubwa.

"Kuwatua kinamama ndoo na mzigo wa kuni, hii si kazi ndogo na haya ni mafanikio makubwa katika maisha ya Watanzania. Ninyi mnajua kinamama wakirahisishiwa kazi hii nchi itapiga hatua kubwa, nguzo ya familia ni mama," alisema Kinana.

HABARI KITAIFA

# Watiwa mbaroni kwa tuhuma kukutwa na meno ya tembo

**Na Allan Isack,**
MANYARA



JESHI la Polisi Mkoa wa Manyara limekamata watu wanne kwa tuhuma za kukutwa na kilogramu 29 za dawa za kulevya aina ya mirungi na meno manane ya tembo.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Babati jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) George Katabazi, alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika matukio tofauti.

Kamanda Katabazi alitaja watuhumiwa hao ni Monica Kamili (48) na mwenzake ambaye hakutaja jina lake, wote wanadaiwa kukamatwa wakiwa na kilogramu 29 za mirungi.

"Watuhumiwa wawili walikamatwa kwa pamoja Mei 21, 2024 majira ya saa 11:30 asubuhi katika Kijiji cha Vilima Vitatu, Kata ya Nkaiti, wilayani Babati," alisema.

Kamanda huyo alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa wanasafirisha dawa za kulevya kinyume cha sheria, wakitumia gari aina ya Toyota Succed lenye namba za usajili T 520 DRU.

Katika tukio lingine, kamanda huyo alisema watuhumiwa Richard Lutema (49), mkazi wa Shinyanga, na mwenzake ambaye hakutaja jina, walikamatwa wakiwa na vipande vinane vya meno ya tembo.

"Watuhumiwa wawili wamekamatwa eneo la Mtaa wa Mji Mpya, mjini Babati saa 16:25 jioni Mei 21 wakiwa na vipande hivyo vinane vya meno ya tembo bila kuwa na kibali," alisema Kamanda Katabazi.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, wakati wowote kuanzia sasa wanatarajia kuwafikisha mahakamani watuhumiwa hao wanne, upelelezi wa tukio hilo ukikamilika.

"Ninatoa wito kwa wananchi kuacha kujihusisha na biashara haramu za dawa za kulevya na nyara za serikali kwani polisi hatutafumbia macho matukio ya uhalifu," alisema Kamanda Katabazi.

Pia alitoa rai kwa jamii kuendelea kuelimisha wananchi na kuendelea kuliamini Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za matukio ya uhalifu ili hatua za kisheria zichukuliwe.

**GARI LA MIRUNGI**

Mkoani Shinyanga, mwandishi wetu Marco Maduhu anaripoti kuwa Jeshi Polisi limekamata gari aina ya Nissan lenye usajili namba T.575 CAF lililosheheni dawa za kulevya aina ya mirungi viroba 25 huku dereva akitokomea kusikojulikana.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema jeshi hilo linaendelea kumsaka dereva wa gari hilo pamoja na mmiliki wake ili kujibu tuhuma za usafirishaji wa dawa hizo.

# Laini za simu 17,000 za 'tuma kwenye namba hii' zafungiwa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema zaidi ya laini za simu 17,300 zimefungiwa kupokea na kutoa mawasiliano kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kujihusisha na uhalifu mtandaoni katika kipindi cha miezi mitatu.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Mwenendo wa Sekta ya Mawasiliano iliyotolewa na TCRA, matukio ya ulaghai yamepungua kutoka laini 20,939 zilizofungwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka 2023 hadi 17,318 Januari hadi Machi mwaka huu sawa na kupungua kwa asilimia 15.

Akizungumzia mwenendo huo, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema kupitia ripoti inaonyesha kuwa hadi kufikia Machi 2024, mikoa ya Rukwa na Morogoro ilikuwa inaongoza kwa matukio ya simu za ulaghai kwa kuwa na theluthi mbili (2/3) ya matukio yote.

Alisema mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Tabora inafuata kwa matukio machache ya ulaghai. Maeneo mengine yalikuwa na matukio machache zaidi ya ulaghai kwenye simu, hasa mikoa ya Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

Dk. Bakari alisema TCRA imebaini simu za ulaghai zinazoingia nchini na hatua stahiki zinachukuliwa. Idadi ya simu za udanganyifu pia imeendelea kupungua.

"TCRA imesimamia katika kuzuia matumizi ya simu zilizoripotiwa kuibiwa, kupotea au kuharibika pamoja na kuzuia matumizi ya simu zisizokuwa na viwango au za bandia. Usimamizi huu unawezesha kubaini na kufungia namba tambulishi za vifaa vya mawasiliano zilizonakiliwa (Duplicate IMEIs).

"Namba tambulishi za vifaa vilivyotumika kwenye udanganyifu pamoja na namba tambulishi zilizotolewa taarifa ya kupotea au kuibiwa," alifafanua.

Alisema TCRA imeendelea kuhimiza wananchi kuendelea kuripoti kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS) simu zote zenye viashiria vya ulaghai au utapeli kwa kutuma namba husika (za matapeli) kwenda namba 15040 bila malipo.


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

## TANGAZO LA NAFASI ZA MASOMO

**UTANGULIZI**

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Ujenzi. Taasisi inawatangazia wananchi wote nafasi za masomo katika Program za Stashahada (Diploma) pamoja na Elimu ya Ufundi Stadi (VET) kwa mwaka wa masomo 2024/2025.

**A. Program za Stashahada**

Mafunzo yanayotolewa katika program ya Stashahada (Diploma) ni kama ifuatavyo:
i. Stashahada ya Uhandisi Ujenzi (Civil Engineering)
ii. Stashahada ya Uhandisi Umeme (Electrical Engineering)
iii. Stashahada ya Uhandisi Mitambo (Mechanical Engineering)

**1. Sifa za Kujiunga na Masomo**

Sifa za kujiunga na masomo katika program za Stashahada (Diploma) ni kama ifuatavyo:
i. Muombaji awe na Cheti cha kidato cha nne (Form IV) chenye ufaulu angalau alama `D` katika masomo ya Hisabati (Mathematics), Fizikia (Physics) au Engineering Science, Kiingereza (English) na Somo lingine lolote ambalo siyo la dini. au
ii. Muombaji awe na Cheti cha Elimu ya Ufundi Stadi daraja la tatu (NVA level 3) au `trade test` daraja la kwanza vinavyotolewa na VETA pamoja na Cheti cha kidato cha nne chenye ufaulu wa angalau alama `D` mbili za masomo yoyote yasiyo ya dini.

**B. Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET)**

Mafunzo ya Ufundi Stadi yanatolewa kuanzia daraja la kwanza (level 1) hadi daraja la tatu (level 3) katika fani zifuatazo:
i. Umeme Magari (Auto Electric)
ii. Umeme wa Majumba (Domestic Electrical Installation)
iii. Ufundi Magari (Motor Vehicle Mechanics)
iv. Ufundi Bomba (Plumbing and Pipe Fittings)
v. Ujenzi na Matengenezo ya Barabara (Road Construction)
vi. Uungaji na Uchomeleaji Vyuma (Welding and Metal Fabrication)
vii. Ufundi Uashi (Masonry and Brick Laying)
viii. Uchoraji wa Ramani za Nyumba (Civil Draughting)

**2. Sifa za Kujiunga na Masomo**

Muombaji anatakiwa awe na Cheti cha kidato cha nne (Form IV) kutoka kwenye Taasisi au Shule yoyote inayotambulika na Serikali.

**C. Mwisho wa kupokea maombi**

3. Kwa Program za Stashahada, mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 13 Septemba 2024.
4. Kwa Elimu ya Ufundi Stadi (VET) mwisho wa kupokea maombi ni
i. Tarehe 28 Juni,2024 kwa `Level III na
ii. Tarehe 30 Oktaba,2024 kwa `Level` I

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KUPITIA**
**MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**
**ICoT**

**S.L.P 963,**
**MOROGORO-MAIN CAMPUS**
**Simu : 023-293 5229/023-293 5226**
**: 0653 456 345, 0686 220 590**
**: 0686 220 590 / 0759 077 606 / 0715 972 010**
**Nukushi : 023-293 5227**
**Barua pepe : mwti@morogoro.net**
**Tovuti : www.icot.ac.tz**

**S.L.P 1957,**
**MBEYA**
**Simu : 025-295 7484/5**
**: 0764 775 354/ 0769 317 404/ 0765251509**
**Nukushi : 025- 295-7486**
**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz/ attimbeyafrica@gmail.com**
**Tovuti : www.icot.ac.tz**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wapigaji na waomba kura, jaribuni tiba ya Askofu Shoo

NI mara nyingine Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, kama alivyo kawaida yake, nyeusi anaitaja nyeusi na nyeupe ataiita nyeupe, kawarushia kombora viongozi wa kisiasa kuhusu uhalisia wao kwa umma uliowapa idhini kushika nafasi hizo.

Pia, akageuza uso kwa umma huohuo, akiufungua macho na kuupatia ujasiri kuwarejeshea ama haki au na adhabu ya kisiasa waliowachagua kulingana na matendo yao kazini, nyenzo kuu akiitaja kura zao katika uchaguzi.

Tunafahamu mwaka huu utamalizika kwa kushuhudia uchaguzi wa ngazi ya mitaa, unaotupatia viongozi wa ngazi ya mtaa, mathalan wenyeviti, vivyo hivyo mwaka ujao, uchaguzi mkuu utaaga kwa kuwaacha madarakani; rais, wabunge na madiwani.

Katika lugha rahisi, umefika muda wa kutosha kujua kiongozi alichopanda mbele ya wapigakura zake, akiangukiwa na jawabu la 'mtu kuvuna alichopanda.'

Hayo yanafanyika, huku nadharia za sayansi ya siasa inasimamia sifa mojawapo ya kiongozi awe amechaguliwa au kuteuliwa, anapaswa 'kukubalika'. Ni wasifu unaomwezesha asonge vyema na jukumu lake ambalo nalo linabeba sifa na tafsiri ya nafasi yake 'kuwaonyesha njia wafuasi wake.'

Hiyo nayo katika upande wa pili wa shilingi ni kwamba, si rahisi kwa kiongozi kukubalika na umma anaouongoza kufuata njia anayowaonyesha, iwapo hawakubaliki kwa tabia na matendo yake. Anaweza kutumia nguvu na mbinu nyingi, lakini akikosa sifa hiyo ya kukubalika inakuwa vigumu kufanikisha.

Turejee darasani tena katika hilo, wataalamu wa sayansi ya Fizikia wana kanuni "ili jambo litendeke, nguvu inapotumika kusukuma na kinachosukumwa kikasogea, hapo kuna kazi inakuwa imefanyika". Au tukidadavua katika lugha yake ya kisomi chenywe "Work done = force times distance moved."

Nadharia hiyo, ndio inaangukia katika darasa la Askofu Shoo wikiendi iliyopita katika staili yake ya kutopindisha sentensi, akatolea uvivu mienendo ya baadhi ya viongozi anaowatuhumu kula rushwa na wabinafsi.

Huku akiweka wazi wasifu muhimu wa kiongozi ni kumcha na kumuogopa Mungu, anatafsiri nyendo hizo hasi ni sumu kubwa kwa umma wanaouongoza kwa kuwaonyesha njia na wakati huohuo, wakitarajia wakubalike kwao. Yaleyale ya fizikia, nguvu inaweza kutumika, lakini manufaa ni pale hatua inapigwa.

Hiyo ilikuwa katika kilele cha siku ya CCT uliofanyika mkoani Mtwara wikiendi iliyopita, akihoji; "Tunataka Tanzania ya namna gani miaka 100 baada ya waliopo kuondoka?

"Viongozi wabinafsi tulio nao ambao wanataka Tanzania iwe mali yao, chochote kinachopatikana ni kwa ajili yao na familia yao, kina 'hohehahe watajiua'..."

"Viongozi waadilifu, wacha Mungu, hawa ndio tuwasukume, tuwaache wagombee ...ndio viongozi wazuri wanaofaa," akafafanua.

Nadhani hayo ya Askofu Dk. Shoo tukiamini na kundi lingine la wafuasi wa dhana hiyo, ni darasa tosha katika nafasi kuelekea uchaguzi, viongozi na kofia zao - vyama vya siasa, kumalizia hatua inayofuata ya utekelezaji.

Ni bahati katika nafasi ya kauli, kuna vyama vya siasa tunavisikia vinalitekeleza hilo. Wakati fulani tukasikia mshikemshike na ukali wa chama tawala CCM kiking'aka juu ya harufu ya rushwa katika nyendo zake za uchaguzi.

Mbali na Mwenyekiti wake, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuikemea, aliyekuwa Katibu Mkuu, Daniel Chongolo akawa 'mbogo' katika vidokezo hivyo vya Dk. Shoo.

Wapinzani wakuu, CHADEMA, hali kadhalika mchakato wa ndani kupata viongozi wa chama umekuwa na umakini na ukali hadi sasa unaendelea wako katika mstari huo kutaka kuwa na kiongozi msafi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# UDSM yatisha Kiswahili muhadhara MV Bukoba

Na Christina Mwakangale

**WIKI** iliyopita, wanazuoni walikutana katika kitivo cha kuwapika na kuwazalisha ambacho ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), chenye sifa lukuki na historia zaidi ya umri wa zaidi ya nusu karne.

Kimetoa wasilisho la kisomi kwa Kiswahili, kwa kipekee, hadhi ya mihadhara kama hiyo huendeshwa kwa lugha ngeni. Kiswahili kikiwekwa kando. Pongezi kwa UDSM pamoja Profesa Rwekaza Mukandala, mwasilishaji mkuu.

Ikumbukwe mihadhara hiyo ya kisayansi au kisiasa, ambayo pengine huchukua takribani miaka 45, kusikika kutoka kwa Profesa aliyetumikia chuo fulani, hutumia Kiingereza.

Kwa UDSM huu ni mhadhara wa tatu, tangu idara inayoshughulikia masuala hayo, ianzishwe Julai, mwaka 1964. Huku wa mwisho ukiwasilishwa mwaka 1979.

Profesa Rwekaza Mukandala, mwanazuoni, mtafiti, mwalimu na kiongozi aliyebobea katika falsafa ya utawala wa kidemokrasia na umma pamoja na siasa linganishi, ndiye aliyekuwa mwasilishaji mkuu katika kusanyiko hilo.

Muhadhara wa Uprofesa, uliandaliwa na UDSM, unamshirikisha Mkuu wa Chuo, Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, wanazuoni wa kada tofauti, wanafunzi, wanasiasa, mabalozi, wanasheria na waandishi wa habari.

Upekee wa kusanyiko hilo, ulinogeshwa na watoa mada, achilia mbali mhusika mwenyewe, akiidadavua meli ya MV Bukoba, yenye historia ya miaka 28, tangu izame na kile kilichokuwa ni wingu zito lililokuwa limeifunika.

Mbinu za uwasilishaji, zikivuta hisia: 'Dola, soko na kushindwa kwa taasisi: Mafunzo katika kuzaliwa kwa uchungu na kushinikizwa. Anakitaja kifo cha mateso na maumivu cha MV Bukoba...'

Awali, kabla ya Prof. Mukandala, kuukumbusha umma kuhusu meli hiyo, iliyoacha makovu miongoni wa walioathiriwa na tukio la Mei 21, mwaka 1997, mwanazuoni mwenzake, Prof. Palamagamba Kabudi, anatia fora, akimpamba mwenziwe.

Prof. Kabudi, alikuwa na jukumu la kuwasilisha wasifu wa Profesa Mukandala. Matamshi yake, mtiririko na mpangilio wa maneno na 'toni' yake viliwakosha wafuatiliaji wa kongamano hilo.

Akatumia maneno ambayo ni nadra kuyasikia kwenye mazungumzo pia kuandikwa yote hayo yakikienzi Kiswahili, mathalani.

"Profesa Mukandala, alikuwa mudiri, mtiva" Yote yakiibua kicheko Nkurumah ukumbi uliosheheni ngano za kitaaluma UDSM.

"Profesa Mukandala, amepitia hatua zote hapa UDSM. Amekuwa Mudiri wa Idara ya Siasa na Utawala. ...Mtiva wa Kitivo cha Sayansi Jamii. Amekuwa Naibu na Makamu wa Mkuu wa Chuo.

"Hakuna Rasi wa Ndaki ya Sayansi ya Jamii, kwa sababu wakati huo, hapa kuwa na Ndaki. Na neno Rasi, kwa mujibu wa Profesa Mulokozi, alilipata katika kamusi iliyoandikwa na Johnson, mwaka 1935," Prof. Kabudi anaendelea kuunakshi wasifu wa msomi mwenziwe.

"Neno ambalo alilitoa katika lahaja ya kimvita inayozungumzwa Pwani ya Kenya, hadi Tanga,"

anasema na kuongeza kuwa Prof. Mukandala ni mlezi wa vyuo vingine. Kikiwamo Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu Muhimbili (MUHAS) na UCLAS hadi kuwa Ardhi University, amekuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Afrika Mashariki Uongozi Institute.

Kadhalika, anamtaja Prof. Mukandala kuwa na machapisho 18, makala vitabuni, majarida ndani na ya kimataifa 51 huku mada maalumu 20, achilia mbali ripoti za ushauri zipatazo 41.

"Profesa Mukandala ana mchango mkubwa katika kukuza demokrasia na Utawala Bora, Tanzania na Afrika Mashariki, Mwenyekiti wa REDET. Kama ipo taaluma ya Sayansi ya Siasa Tumizi (Applied Political Science), kwa eneo letu la Afrika, gwiji na kinara ni Profesa Mukandala.

"Maprofesa wengi waliahirisha kufanya mhadhara kama huu, kutokana na shughuli nyingi. Profesa Mukandala akiweka akiba ya kutosha, ili aitumie sasa kuuwasilisha kwa Kiswahili, kwa sababu angewasilisha mwaka 1997, angetumia Kiingereza."

"Profesa Mukandala, mmoja wa 'hidaya' au zawadi kitaaluma kwa Tanzania, Afrika na Afrika Mashariki. Atatumia mbinu anuai, fizikia, sheria na uchumi, siasa, hadi kuhitimisha, tangu 'kuzaliwa kwa uchungu na kushinikizwa; kifo cha mateso na maumivu cha MV Bukoba'.

## Profesa Mihanjo: Nchi za Afrika ziwe na sauti moja kiusalama

**Na Mwandishi Wetu**

PROFESA Eginald Mihanjo anayefundisha masomo ya kimkakati katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) amesema katika kuadhimisha miaka 20 ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika (AU), kuna haja nchi za Afrika kuwa na sauti na nguvu moja ya kuhakikisha zinakuwa huru.

Jijini Dar es Salaam wakati wa kongamao maalum lilioandaliwa na Taasisi ya Uongozi kwa ajili ya kujadili masuala ya ulinzi na usalama kwa nchi za Afrika mwishoni mwa wiki, Prof. Mihanjo alisema nchi hizo zikishikamana na kuwa huru zitasaidia kwa kiasi kikubwa utulivu na amani, hivyo milio ya risasi kutosikika mahali popote.

Alisema nchi za Afrika zimejikomboa kiuchumi licha ya changamoto za kiusalama zilizopo. Zikiungana na kuwa na sauti moja zitasaidiana kuwa huru.

"Tunapoongelea masuala ya mabadiliko yasiyokuwa ya kikatiba katika nchi zetu, inapaswa tuyaondoe na kuweka nguvu za pamoja katika kuimarisha sekta za kijamii," alisema.

Prof. Mihanjo alisema zaidi ya asilimia 50 ya watu ifikapo mwaka 2025 watakuwa vijana, hivyo ni muhimu kubeba kundi hilo husussan walio chini ya miaka 25 kwa nchi za Afrika kuhakikisha wanawekewa mazingira mazuri ya ajira.

Brigedia Jenerali Paul Mella alisema jukumu la kulinda amani na kuhakikisha nchi za Afrika zinakuwa salama ni la kila mmoja na si la wanajeshi peke yao.

"Afrika inahitaji ushirikiano wa nchi na nchi kuhakikisha maeneo yote yenye changamoto za kiusalama zinatatuliwa kwa ushirikiano wa kikanda.

"Ushirikiano wetu kama Afrika ni njia mojawapo ya kupambana na matatizo mbalimbali ya kiusalama kwa kuwa dunia hii si salama sana, ni duniani ambayo iko katika mpito, inatoka katika dunia iliyotawaliwa na mfumo wa dola moja yenye nguvu na kwenda katika mfumo mwingine ambao ni pande mbili au tatu," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. William Anangisye alisema kongamano hilo limetoa nafasi kwa vijana wa chuo kikuu na Watanzania kujifunza na kuuliza maswali yanayohusu ulinzi na usalama wa Bara la Afrika.

Alisema Tanzania imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha ulinzi na usalama ni sehemu ya maisha ya Watanzania, ndio sababu kuna kipindi serikali inatuma jeshi katika nchi mbalimbali kuhakikisha ulinzi na usalama unapatikana.




Naibu Waziri wa Maji, Kundo Mathew (kushoto), akizungumza baada ya kuzindua ujenzi wa mradi wa maji kwenye kijiji cha Sokoine Ranchi unaogharimu Sh. milioni 348 na kuwaepusha wananchi kunywa maji ya madimbwi yanayochangiwa na ng'ombe. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Wananchi wapewa elimu ya fedha kuepuka mikopo umiza

**Na Josephine Majula,**
KAGERA

WANANCHI wilayani Bukoba, mkoani Kagera wameshukuru serikali kwa kufikisha huduma ya elimu ya fedha, wakiamini italeta mabadiliko kiuchumi na kuepusha upotevu wa fedha.

Wakizungumza juzi kwa nyakati tofauti baada ya kupata elimu hiyo, wananchi hao, akiwamo mfanyabiashara Ivona Gasper, walisema watawaeleza wenzao kile walichofundishwa ili wawe na uelewa mpana juu ya masuala ya fedha.

"Tunaiomba serikali iendelee kutoa elimu ya fedha kwa wananchi wake na kuhakikisha inawafikia watu wote nchi nzima kwa sababu wananchi wengi wanapoteza fedha kwa kukosa elimu," alisema Ivona.

Mwelimishaji Rika Ngazi ya Jamii, Jackline Petro, alisema kuwa baada ya kupata elimu ya fedha, amejua sehemu sahihi ya kutunza fedha zake kama vile benki, vyama vya akiba na mikopo (SACCOS) na vikundi vidogo vilivyosajiliwa.

**Wakizungumza juzi kwa nyakati tofauti baada ya kupata elimu hiyo, wananchi hao, akiwamo mfanyabiashara Ivona Gasper, walisema watawaeleza wenzao kile walichofundishwa ili wawe na uelewa mpana juu ya masuala ya fedha.**

Ofisa Usimamizi wa Fedha Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha katika Wizara ya Fedha, Stanley Kibakaya, alisema serikali itahakikisha watu wote waliokusudiwa kupata elimu awamu ya kwanza wanafikiwa kama ilivyopangwa.

"Tumejipanga kutoa elimu kwa watu wote, wakiwamo watoahuduma na watumiaji huduma za fedha, ili wawe na uelewa wa pamoja na mambo ya kuzingatiwa kuhusani wakati wa kutoa mikopo au kuchukua mikopo," alisema Kibakaya.

Ofisa Biashara Mkoa wa Kagera na Mratibu wa Huduma za Fedha Ngazi ya Mkoa, Keneth Mlilo, alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa kwa wananchi kujitokeza kupata elimu ya fedha husussan kinamama kwa kuwa imeonekana kundi hilo ndilo waathirika wakubwa wa mikopo umiza yenye riba zisizolipika.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED






Mkuu wa Idara ya Mikopo, Yonah Mgongolwa (kushoto), Mkuu wa Idara ya Wateja Wadogo na wa Kati wa Benki ya Mwanga Hakika, Mwinyimkuu Ngalima (katikati) na Mkuu wa Idara Biashara, Projest Massawe, wakizindua huduma rahisi ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati "Fursa Loan" jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni ya kukusanya bil. 2/- kudhibiti VVU yazinduliwa

**Na Nadhifa Omar,** TACAIDS

KAMPENI maarufu ya kuchangisha fedha za kudhibiti maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI ya Kili Challenge 2024 imezinduliwa ikitarajiwa kukusanya Sh. bilioni mbili.

Ni kampeni inayoratibiwa na Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGML) kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) inayofanyika Julai ya kila mwaka.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa TACAIDS, Jumanne Isango, alisema TACAIDS inaendelea kuheshimu mchango mkubwa unaopatikana kupitia Kili Challenge na itaendelea kudumisha kampeni hiyo.

"Kwa niaba ya wafanyakazi na uongozi wa TACAIDS, GGML, Kamati ya Kili Challenge na Bodi ya Wadhamini ya Kili Challenge na Serikali ya Tanzania tunawashukuru kwa kuendelea kuunga mkono mpango wa kupanda Mlima Kilimajaro. Madhumuni ya Kili Challenge ni kuchangisha fedha na uhamasishaji kudhibiti VVU na UKIMWI.

"Kwa pamoja tufanye mpango huu uendelee kuwa shirika la hisani la sekta ya umma na binafsi dhidi ya VVU na UKIMWI katika Afrika Mashariki. Kwa mwaka huu tunatarajia kuwa kampeni hii itakusanya Sh. bilioni mbili, hivyo tuendelee kuunga mkono," alisema Isango.

Akizungumzia mgawanyo wa fedha hizo, Isango alisema: "Kila siku na kila mwaka, fedha hizi zinazopatikana kupitia mpango huu zimekuwa zinaleta athari chanya kwa jamii.

"Hadi sasa kupitia Kili Challenge, tumefanikiwa kuchangia zaidi ya asasi 22 za ndani na taasisi kadhaa za serikali na kuwanufaisha mamilioni ya Watanzania.

"Hili limewezekana kupitia michango ya hisani na msaada kutoka kwa wadau mbalimbali wanaofanya kampeni hii kuwa mfano ambao sote tunajivunia," alisema Isango.

Vilevile, Isango ambaye alimwakilisha Kaimu Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela, alimshukuru Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle kutokana na mchango mkubwa ambao umekuwa ukitolewa na PEPFAR.

"Kuwapo kwako hapa leo Mheshimiwa Balozi, kunaashiria kuunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI nchini.

"Tunashukuru kwa msaada mkubwa kutoka kwa PEPFAR na mashirika mengine yote ya Serikali ya Marekani kwa miongo kadhaa sasa tangu janga la VVU kuibuka katika nchi yetu tunapoadhimisha miaka 22 tangu kuanza kwa Kili Challenge," alisema Isango.

**HALI YA VVU/UKIMWI**

Kuhusu hali ya VVU na UKIMWI nchini, Isango alisema kuwa fursa hii hutoa mambo muhimu kuhusu hali ya VVU na UKIMWI katika nchini.

Alisema kwa mujibu wa THIS 2022/23, Tanzania ina watu 1,548,000 wanaoishi na VVU (WAVIU). Maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 16.7 kutoka watu 72,000 (THIS 2016/17) hadi 60,000 (THIS 2022/23).

Akizungumza kuhusu wapandaji mlima, Isango alisema, "Kwa wapandaji wetu wachangamfu kwa mwaka huu, ambao wataziacha familia zao nyuma na kukabiliana na changamoto ya kupanda milima na miteremko ya Kilimanjaro, tunasema 'ninyi ndio mnaleta mabadiliko', hivyo tunajivunia uamuzi wenu ambao unaleta furaha kwa Watanzania wengine .

"TACAIDS itaendelea kuimarisha dhamira yake ya kuifanya Kili Challenge kuwa kipengele cha kudumu katika shughuli zetu za Tanzania, tunafungua mikono yetu kwa ushirikiano zaidi na kampuni zote ambazo zinawajibika kwa matumaini na mustakabali mzuri wa taifa hili."

Alisema jitihada za pamoja zinahitajika kutimiza lengo la kutokomeza VVU na UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

Awali Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti wa Masuala ya Uendelevu na Mambo ya Ubia (Afrika), Simon Shayo, alisema vikundi mbalimbali vimefaidika na kampeni hiyo, ikiwa ni pamoja na watoto wa Kituo cha Watoto Yatima cha Moyo wa Huruma, ambacho pia kinawatunza watoto wengine walio katika mazingira magumu.

"Kundi la kwanza la watoto waliokulia katika kituo hicho sasa wanasoma vyuoni, wakiwamo wawili wanaosoma digrii za udaktari," alibainisha Shayo.

Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle alisema kuwa hivi sasa wako katika hatua ambayo uendelevu ndio ufunguo wa mafanikio ya muda mrefu ili kudumisha mafanikio yaliyopatikana chini ya PEPFAR huku akisisitiza kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

"Uendelevu ni muhimu kwa sababu kadhaa muhimu. Kwanza, PEPFAR haikukusudiwa kuwa suluhisho la kudumu; ilikusudiwa kushughulikia hitaji la dharura. Tanzania imepiga hatua kubwa katika kudhibiti janga la UKIMWI. Viwango vya maambukizi mapya vimepungua kwa kiasi kikubwa, kama vile vifo vinavyohusiana na UKIMWI.

"Pili, Tanzania iko kwenye njia nzuri kuelekea kuwa nchi ya kipato cha kati. Kwa maendeleo haya, Tanzania itazidi kuwa na uwezo wa kushughulikia mahitaji yake ya afya.

"Moja ya vipaumbele vyangu kama Balozi wa Marekani nchini kimekuwa kuimarisha uhusiano mkubwa wa kibiashara ili kufikia malengo yetu ya pamoja. Nina furaha kuona ushirikiano uliopanuliwa kati ya sekta ya afya ya Marekani na Tanzania. Sekta ya binafsi itakuwa muhimu katika awamu inayofuata ya juhudi zetu za kuzuia maambukizi ya VVU na matibabu ya UKIMWI," alisema Balozi Battle.

Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Duan Archery, alisema, "Michango yenu ni ya thamani kubwa na itatusaidia kufikia lengo letu la 'kufikia sifuri'."

Malengo matatu ya sifuri ni kutokuwapo maambukizi mapya, kutokuwapo ubaguzi na kutokuwapo vifo vinavyotokana na UKIMWI.

Kwa mujibu wa Archery, mwaka huu wanatarajia kuwa na washiriki 60; wapandaji mlima 42 na waendesha baiskeli 18. Wawili kati ya washiriki hao ni watoto wadogo, mvulana na msichana kutoka Kituo cha Watoto Yatima cha Moyo wa Huruma cha Geita, ambacho kilianzishwa mwaka 2006 kwa ufadhili kutoka Kilimanjaro Challenge.

Kilimanjaro Challenge ilianzishwa mwaka 2022 chini ya uratibu wa GGML na TACAIDS kwa lengo la kuchangisha fedha za mwiitikio wa UKIMWI. Fedha hupatikana kutokana na kupanda na kuzunguka Mlima Kilimanjaro kila mwaka. Washiriki hununua tiketi za Challenge kama sehemu ya kampeni yao ya kuchangia fedha.

Wakati baadhi ya ada inagharamia kupanda mlima na kuendesha baiskeli, sehemu kubwa ya fedha inaingia kwenye Kili Trust Fund na hutumika kusaidia mapambano ya kitaifa dhidi ya UKIMWI. Mfuko wa Kili ni mchangiaji mkuu wa Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI.

## Benki ya Mwanga Hakika yazindua mikopo kwa wajasiriamali nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuwezesha biashara nchini, Benki ya Mwanga Hakika imeleta sokoni huduma ya mikopo rahisi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ili kuwakwamua kiuchumi ijulikanayo kama Fursa Loan.

Huduma hiyo inakuja wakati ambao Watanzania wengi wamekuwa wanahitaji huduma za mikopo yenye riba nafuu na dhamana zinazoendana na aina ya biashara zao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo wiki iliyopita, Mkuu wa Wateja Wadogo na wa Kati wa Mwanga Hakika Bank, Mwinyimkuu Ngalima, alisema benki hiyo imejizatiti katika kuleta huduma zinazokidhi mahitaji ya makundi mbalimbali ya wateja.

"Tunafarijika kuja na huduma hii ya mkopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ambayo ni mikopo yenye gharama nafuu na dhamana zake zinalingana na aina ya biashara zao.

"Tunaamini huduma hii inakwenda kuwa msaada mkubwa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kama mamalishe, bodaboda, madereva wa magari madogo ya biashara na wengineo ambao wamekuwa wanashindwa kupata mikopo kutokana na gharama kubwa na  kutokuwa na dhamana," alisema.

Ili mteja aweze kupata mkopo kwenye benki, anahitaji kuwa na dhamana ya mali isiyohamishika kama vile nyumba zenye hati miliki au mashine (kiwanda) jambo ambalo limekuwa likiwakosesha mikopo wafanyabiashara wadogo wasio na dhamana hizo.

Alsiema huduma hiyo inatoa fursa ya kipekee kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati kupata mikopo yenye gharama nafuu na dhamana rahisi itakayowawezesha kuongeza mitaji kwenye biashara zao ili zikue zaidi.

"Tunawakaribisha wajasiriamali wote bila kujali aina ya biashara kutumia fursa hii ili wakukuze biashara zao kwa kuongeza mitaji," alisema.

Tanzania inakadiriwa kuwa na biashara ndogo na za kati takribani milioni tatu zinazochangia Pato la Taifa kwa asilimia 27. Sekta hiyo pia ni muhimu katika kufikia maendeleo endelevu nchini ikichangia katika ajira na ubunifu.

Mteja anaweza kupata huduma hiyo kupitia tawi lolote la Benki ya Mwanga Hakika nchini.

Ili kuipa thamani zaidi, benki hiyo imekuja na huduma ya ziada ya akaunti ya malengo (Fulsa saving account) itakayowawezesha wafanyabiashara wadogo kutunza fedha kwa malengo ya baadaye.



# Makonda: Sitishwi na kelele za mitandaoni

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amewajibu wanaomshambulia katika mitandao ya kijamii, akisema hatishwi na kauli hizo, kwamba ni sawa wanabembeleza na kumwongezea nguvu katika utendaji kazi wake.

Alitoa kauli hiyo jana akiwa kwenye ziara Wilaya ya Monduli mkoani Arusha kwa ajili ya ukaguzi wa miradi na kutatua kero za wananchi.

"Nasikia kuna watu wanahangaika mitandaoni, ni kama wananipigia mdundo yaani na umri huu nitishike na kauli za watu? Ulishawahi kwenda kwenye chumba cha massage halafu ukawekewa kale kamziki inakuwa kama rhythm. Sasa mimi ndio ninavyojisikia," alisema Makonda na kuongeza:

"Wanavyoendelea kutoa hizo kauli mimi nasikia hiyo hali ya kunibembeleza ikiniambia nenda Makonda endelea na leo (jana) nipo Monduli kuwapiga spana wavivu wote hatuwezi kwenda hivyo."

Aidha, alimwomba Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Festo Kiswaga, kusimamia miradi na asisite kuwachukulia hatua wanaohusika na ubadhirifu.

"Mfahamu miradi isipotekelezwa ndani ya muda hawa makandarasi kuna namna wanaongeza gharama ambayo ni maumivu kwa mwananchi yaani mwananchi ateseke miaka yote tumepewa upendeleo wa shule ya wasichana ili kuondoa mimba za utotoni ipo Longido, ili mradi ukamilike tunatakiwa kuwa na fedha ya ziada inatoka wapi?," alihoji Makonda.

**Aidha, alimwomba Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Festo Kiswaga, kusimamia miradi na asisite kuwachukulia hatua wanaohusika na ubadhirifu.**

Makonda amesema: "Ukishafika Monduli upande mmoja una Edward Sokoine na upande wa pili ni kuna Edward Lowassa halafu unakuwa muoga, ninaomba mwendelee kunipigia mdundo... wale mnaotoa kauli mnanisaidia kufanya kazi kwa molari kubwa."

Amesema kuna siku alieleza umoja wa waovu, wala rushwa na wazembe ni mkubwa sana.

Makonda alisema: "Ukitaka kujua kama upo mguse mvivu mmoja utaona wavivu wote wanajitokeza au mguse mla rushwa mmoja wala rushwa wote wataibuka."

Aliongeza: "Nawaambia tena nitawapiga spana na mnavyojitokeza tunapata nafasi ya kujua kumbe naye huyu yumo...alizalilishwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti wa CCM, mwanadiplomasia namba moja, mama mwenye familia katukanwa asubuhi hadi asubuhi sijasikia kauli ya mtu yoyote sisi wanaume tulijitokeza kumpiganía yule mama."

Alisema: "Leo mzembe mmoja mla rushwa mmoja mnapiga kelele huko ebooo!" Amesema Makonda.

Aidha, Makonda alisema wapo watumishi wilayani Monduli waliokusanya fedha za ushuru na hazijulikani zilipokwenda akisema atamalizana nao.

Alisema tayari amemwelekeza Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha kama mtumishi hawezi kufanya kazi inavyotakiwa aandike barua ya kuhama, watamsaidia aondoke.

Makonda alisema: "Mkuu wa Wilaya simamia bila kutetereka na bahati nzuri bosi wako ni mimi kila mmoja ataripoti kwa bosi wake. Tukicheka cheka hivi itafikia hatua kuna miradi ambayo itakuwa haiendi mtumishi yoyote hakikisha anakupa matokeo."

## NPS yapokea mashauri 22 ya ukatili wa kijinsia

**Na Steven Williamm,** MUHEZA

OFISI ya Taifa ya Mashtaka (NPS) katika Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, imepokea mashauri ya jinai 22 yanayohusiana na ukatili wa kijinsia, ubakaji na ulawiti kwa kipindi cha miezi 10.

Kesi hizo ni zile zilizosajiliwa na NPS, kuanzia Aprili mwaka jana hadi Mei mwaka huu.

Mkuu wa NPS, wilayani humo, Petrida Muta, alisema jana kuwa kesi za ubakaji ziliripotiwa 13, ulawiti kesi nane, huku kesi za unyanyasaji wa kingono zikiongezeka kwa kasi.

Kwa sasa, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ya Taifa katika Mkoa wa Tanga, zimefunguliwa katika Wilaya za Handeni, Muheza, Lushoto na Tanga.

Katika Wilaya ya Muheza, tangu kufunguliwa kwa ofisi hiyo ya mashtaka kwa mara ya kwanza amehukumiwa kwenda jela kifungo cha maisha Ramadhani Iddi (46), mkazi wa Kilapula, Kata ya Ngomeni, aliyetiwa hatiani kosa la kumlawiti mtoto wa miaka 13.

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeanzishwa kama Ofisi huru ya umma kupitia Tangazo la Serikali Na.49 la Mwaka 2018 la tarehe 13 Februari, 2018 la kuanzisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kwa ajili ya kutekeleza mamlaka ya kikatiba.

Kwa mujibu wa Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Mkurugenzi wa Mashtaka amepewa uwezo na mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa mashtaka yote ya jinai katika mahakama zote isipokuwa mahakama za kijeshi.

Kwa msingi huo, Mkurugenzi wa Mashtaka ana uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote ya jinai nchini.



Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Serapion Bashange, akitoa taarifa kuhusu hali ya elimu katika wilaya hiyo kwenye kikao cha wadau wa elimu kilichofanyika juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Halmashauri yafuta wazo la kuanzisha shule ya kiingereza

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, imefuta wazo la kuanzisha Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza, baada ya kushauriwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dionis Myinga, alisema serikali imezuia uanzishaji wake kwa sababu shule nyingi zilizoanzishwa zinatumia rasilimali za shule za kawaida za msingi za serikali.

Myinga alitangaza uamuzi wa kufuta wazo hilo la kuanzisha shule hiyo katika kikao cha robo ya tatu ya mwaka kilichofanyika juzi.


"Baada ya kushauriana na wizara, sisi kama halmashauri tumeafiki ushauri wa serikali kupitia TAMISEMI na sasa tumeondoa wazo hilo," alisema.

**Kwa mujibu wa Myinga lengo lingine lilikuwa ni kuiongezea halmashauri hiyo mapato kupitia ada za wanafunzi na kushindana na sekta binafsi katika taaluma.**

Alisema Hai ilipanga kuanza na wanafunzi wa darasa la kwanza 45 sawa na mkondo mmoja na wanafunzi wa awali 90.

Miyinga alisema lengo kubwa la kuanzisha shule hiyo ya mchepuo wa kiingereza ilikuwa ikilenga kuwasaidia wananchi wa Hai, ili kuhakikisha wanapata nafasi ya kuwasomesha watoto wao katika shule nzuri kutokana na uhitaji wa shule za aina hiyo kuwa mkubwa.

Kwa mujibu wa Myinga lengo lingine lilikuwa ni kuiongezea halmashauri hiyo mapato kupitia ada za wanafunzi na kushindana na sekta binafsi katika taaluma.





# Chemchemu ya matope yaibuka eneo la mnada

**Na Marco Maduhu,**
KISHAPU

CHEMCHEMU iliyoambatana na matope imeibuka katika eneo panapotekelezwa ukarabati wa mnada wa Mhunze wilayani Kishapu unaogharimu zaidi ya Sh.milioni 710.

Hali hiyo imemshtua Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha na kutaka uchunguzi wa kitaalamu kufanyika, ili kuepuka kuteketeza fedha za serikali katika eneo hilo.

Macha alitoa agizo hilo juzi alipotembelea na kukagua ukarabati huo na kubaini kuwapo kwa chemchemu pamoja na matope kuibuka kutoka ardhini.

Alisema eneo hilo la mnada linajengwa ukuta wa uzio umempa wasiwasi kuwa siyo salama kwa ajili ya shughuli za mnada.

"Nisije kunukuliwa vibaya kwamba Mkuu wa Mkoa amezuia ujenzi wa ukarabati wa mnada hapana. Mimi sijazuia ila natoa ushauri tu wataalamu waje wachunguze juu ya tope linalotoka chini ya ardhi na hii chemchemu kama haviwezi kuleta madhara," alisema.

**Hali hiyo imemshtua Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha na kutaka uchunguzi wa kitaalamu kufanyika, ili kuepuka kuteketeza fedha za serikali katika eneo hilo.**

Aliongeza: "Wakisema hakuna shida basi endeleeni kujenga, wakisema litaleta shida tutafute eneo lingine ili fedha ya serikali isije potea".

Ahmad Abdalah kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ambao ndiyo wanafanya ujenzi wa ukarabati wa mnada huo, alikiri kukabiliana na changamoto mbalimbali likiwamo hilo na kuwa wametumwa wataalamu wa jiolojia ili kupima athari za tope hilo.

Baadhi ya wauzaji wa mifugo kwenye mnada huo walilalamikia uwapo wa tope hilo wakisema mifugo yao mara nyingi imekuwa ikizama, hivyo kutumia gharama kubwa kuitoa ndani ya tope.

Walisema hata wao pia limekuwa likihatarisha usalama wao na kuiomba serikali kama kuna eneo lingine mnada huo uhamie huko.

## Watakiwa kutumia fursa kupaa bei ya asali

**Na Benny Kingson,** TABORA

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Tabora, Asha Churu, amewataka wananchi mkoani Tabora kutumia fursa ya kupanda kwa bei ya asali ili kujikwamua kiuchumi.

Alitoa ushauri huo juzi alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha wakati wa maadhimisho ya Siku ya Nyuki Dunia.

Alisema kuwa Mkoa wa Tabora hususani Manispaa ya Tabora imejikita katika shughuli za uchakataji mazao ya nyuki na kwamba kuna misitu na maeneo ya kutosha.

Alisema kufanya uwekezaji wa mazao yatokanayo na nyuki yana faida kubwa kwa afya za binadamu pamoja na ukuaji wa uchumi.

"Kwa sasa bei ya asali imezidi kupaa ambapo kilo moja ni Sh.10,000 na kwa Dar es Salaam ni kati ya Sh.15,000 hadi Sh. 20,000 na ikipelekwa nje ya nchi bei inapanda zaidi na kuwezesha mhusika kupata faida kubwa," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) mkoani Tabora, Mohamed Wawa, alisema wamejikita kuzalisha wataalamu bora waliobobea ili kuisaidia jamii kufikia malengo ya kuhakikisha zao hilo kuwa juu kibiashara.

Alisema kuwa nyuki anazalisha bidhaa kama asali, nta, gundi, maziwa, supu, sumu na poleni ambazo zote zina kazi yake.

Alisema faida ya asali ni kwa mahitaji ya afya, lishe na tiba ya mwilini na nyingine kuzalisha bidhaa mbalimbali ikiwa ni faida kwa watumiaji na zaidi kuwapatia vipato na kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa.

## Polisi wajibebesha jukumu kuelimisha utapeli wa fedha

**Na Josephine Majula,**
KAGERA

MKUU wa Polisi Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, Jonas Soa, amasema kuwa ni wajibu wa polisi kuelimisha wananchi kuhusu mbinu zinazotumiwa na matapeli kujipatia fedha.

Aidha, amesema kuna umuhimu wa kuwaeleimisha polisi jamii juu ya fedha kwa kuwa wanaishi nao kwenye maeneo yao ambayo itasaidia kupunguza matukio ya watu kutapeliwa.

Pia, ameahidi kutoa ushirikianokwa timu ya wataalam wa Wizara ya Fedha ambao wanafanya kampeni ya kutoa elimu ya feda kwa umma katika mikoa mbalimbali nchini.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na askari polisi katika semina ya masuala ya fedha iliyofanyika katika Kituo cha Polisi Kyaka, pamoja na mambo mengine alisema wataendelea kuwaelimisha polisi wengine ambao hawajafikiwa na elimu hiyo.

Alisema kuwa elimu ikiwafikia wananchi wote nchini itaisaidia serikali kupunguza migogoro ya kesi mbalimbali zinazoendelea kwenye vituo vya polisi kuhusu mikopo inayowakumba wananchi mbalimbali.

Mkaguzi wa Polisi Wilaya ya Missenyi, Baraka Mafwimbo, aliiomba serikali kuongeza nguvu ya kudhibiti na kuimarisha mifumo ya taasisi zinazohusika na utunzaji wa taarifa binafsi za wananchi, kuhakikisha zinalinda taarifa hizo, ili kuepusha taarifa hizo kufikiwa na watoa huduma ya mikopo na kuweza kuwashawishi kukopa fedha.

"Binafsi nimewahi kupigiwa simu na kushawishiwa kuchukua mkopo na watoa huduma ambao sikujua taarifa zangu wamezitoa wapi, lakini walikuwa wananielezea kama wananifahamu, hawakuweza kufanikiwa kwa kuwa nimewahi kupata elimu ya masuala ya fedha zamani," alisema Mafwimbo.

Ofisa Usimamizi wa Fedha Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha, Mary Mihigo, alisema ni muhimu wananchi wakajua kuwa wanapaswa kuomba mikopo kwa taasisi zilizosajiliwa rasmi kuepusha matapeli.

"Utajua kuwa ni taasisi rasmi ya kukopesha, kupitia tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ambayo imeorodhesha taasisi rasmi zote za utoaji mikopo nchini, hivyo ni lazima mwananchi kabla hajakopa kujiridhisha kwenye usajili wa taasisi husika,"alisema Mihigo.

Alisema kuwa Wizara ya Fedha, itaendelea kutoa elimu ya masuala fedha kwa wananchi wa makundi mbalimbali, ili kuhakikisha wanakuwa na uelewa mpana wa masuala ya fedha ikiwemo elimu ya mikataba, uwekezaji na mikopo umiza.



Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha dawa za binadamu zilizomaliza muda wa matumizi paketi 86 katika moja ya duka la dawa Manispaa ya Shinyanga na mtuhumiwa wanamshikilia. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 'Msiogope kuja kupatiwa matibabu hospitali za jeshi'

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WANANCHI pamoja na wakazi wa maeneo mbalimbali jijini Mwanza wametakiwa kutokuogopa kufika katika Hospitali ya Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ) Kanda ya Ziwa ili kujipatia huduma mbalimbali hasa zile za kibingwa.

Wito huo umetolewa na mkuu wa kikosi, chuo na hospitali hiyo, Dk. Luteni Kanali Ahmed Shabhay wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda hospitalini hapo.

Dk.Luteni Kanali Shabhay alisema kumekuwa na kasumba kwa baadhi ya wananchi kuogopa kwenda kupata huduma hospitalini hapo wakidhani ni kwa ajili ya wanajeshi pekee.

**Pia aliwaagiza Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) kufanya upembuzi wa barabara hiyo ili ukarabati wake uanze mara moja.**

Dk. Luteni Kanali Shabhay ambaye ni Bingwa wa Upasuaji alisema hospitalini hapo zinatolewa huduma bora na muhimu na kuwa wanapokea malipo ya moja kwa moja pamoja na malipo ya kupitia bima ya afya.

Pia aliiomba hospitali hiyo iboreshewe miundombinu ya huduma za maji pamoja na barabara ya kuingia na kutokea kwenye kikosi hicho yenye urefu wa km 14.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda alilipongeza JWTZ kwa kuboresha huduma za afya kwa ujenzi wa miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa tiba na vitendanishi, ikiwamo vipimo vya mionzi, X-ray, CT- Scan na huduma za mahututi ambazo zote ni za kisasa.

Pia aliwaagiza Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) kufanya upembuzi wa barabara hiyo ili ukarabati wake uanze mara moja.

Kadhalika, aliiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kuboresha huduma hizo hususani kupitia Mradi wa Maji Butimba eneo la upanuzi wa mradi kwa awamu ya pili.



Ukurasa 12

**Atikisa Moro akiungana na Rais nishati safi jikoni**



Ukurasa 13

Viboko kwa watoto, wanafunzi adhabu inayozidi kulumbaniwa



Ukurasa 14

**Mkono wa taasisi elimu ya juu kuboresha afya ulipoikuna WHO**


Nipashe

# TESA

Jumanne Mei 28, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


ELIMU

NA BEATRICE SHAYO

# Waajiriwa kupoteza haki nyingi kazini kumbe wanapofeli ni hapa

MEI ni mwezi wa kuwaenzi wafanyakazi, tena ukipewa umuhimu zaidi wa kusherehekea Mei Mosi ambayo ni maadhimisho ya siku yao ili kutambua mafanikio na mchango wao kufikia maendeleo.

Katika uwanja wa kazi na ajira suala la mahusiano kazini kati ya waajiri na watumishi ni jambo lisilokwepeka, aghalabu kunyimwa haki na unyanyasaji wa waajiriwa na kuleta migogoro, inayotokea na kuhitaji usuluhishi wa kisheria.

"Ndiyo maana serikali imeunda chombo cha umma cha kutatua migogoro kazini kwa njia za usuluhishi," anasema ya Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Usekelege Mpulla.

Anawakumbusha wafanyakazi kukitumia wanapopata changamoto, akisema ni eneo sahihi la kujibu maswali na matatizo yanayotokea sehemu za kazi.

Akifafanua zaidi, anasema CMA ni chombo cha umma kinachoshughulikia migogoro ya wafanyakazi kwa usuluhishi akisisitiza kuwa ni taasisi pekee kisheria ambayo ni kimbilio la wafanyakazi wanapovunjiwa haki zao.

Mpulla anayasema hayo wakati wa mahojiano na Nipashe jijini Dar es Salaam, kuhusu masuala ya wafanyakazi ambayo yamepewa kipaumbele hasa wakati huu wa Mei Mosi 2024.

Anataja baadhi ya mambo kuwa ni kuachishwa kazi bila kufuata taratibu na wala kuwapo sababu za utoshelezi, kutokulipwa mishahara ama kupewa chini ya kiwango cha kima cha chini kilichopangwa kisheria.

"Kuna mengine kama madai ya likizo na kiinua mgongo, hivyo wafanyakazi wafahamu kuwa CMA ndilo kimbilio ili kupata haki. Kwa kutambua umuhimu wa wafanyakazi na waajiri ambao ni wazalishaji kwa lengo la kukuza uchumi wa taifa."

**MIKAKATI**

Anasema CMA ni taasisi huru inayoshughulika na utatuzi wa migogoro ya kikazi Tanzania Bara kati ya waajiri, waajiriwa na vyama vya wafanyakazi na kwamba ili kutumiza azma hiyo ni lazima kwenda na wakati au kidijitali.

"Moja ya mkakati wetu ni kutumia mtandao kuruhusu wafanyakazi watakaokuwa na kesi kuziwasilisha kwa njia ya mtandao. Tunakuja na mfumo wa Online Case Management System (OCMS). Shauri tutalifanyia kazi na mwajiri atahojiwa kuhusiana na madai yaliyowasilishwa." Anafafanua kuwa wanalenga kumaliza migogoro inawagusa wafanyakazi kwa haraka ili wasitumie muda mwingi kwenye kesi bali utumike zaidi kuzalisha.

Mipango ipo katika hatua mbalimbali na tayari wameanza kusimika mifumo itakapokuwa tayari utawawezesha hata wale walio mbali kuhudumiwa bila ucheleweshaji.

"Ina maana akipata kesi kama ana simu janja ataingia katika mtandao na kuwasilisha taarifa zake kwenye mfumo zitatufikia, tutasajili kesi na kuweka utaratibu wa kuanza kutatua migogoro," anasema Mpulla.

Anasema katika hatua nyingine ukishasajili kesi watakuwa na uwezo wa kutoa taarifa kwa aliyeshtakiwa kwa kuwa mfumo utakuwa na taarifa kutoka kwa aliyefungua shauri.

Anaeleza kuwa atapata taarifa ya kuhusu shauri kufunguliwa dhidi yake baada ya hapo taratibu za kupanga tarehe ya kuanza kusikilizwa pasipo ulazima wa kufika ofisini zitaanza.

Anawaambia wadau kuwa mfumo wa OCMS unatarajia kuanza mwishoni mwa mwezi ujao na kwa sasa upo kwenye hatua ya majaribio ya watumiaji ambao unatarajia kuanza Mei mwaka huu.



Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, Usekelege Mpulla. **PICHA: MTANDAO**

"Kwa sasa tunachokifanya ni kuhakikisha mifumo inasomana kama mlivyomsikia Rais Samia Suluhu Hassan, akisisitiza hilo. Mahakama na taasisi mbalimbali tunazofanya kazi za kufanana lazima mifumo isomane ndicho tunachokifanya baada ya kukamilisha tunaenda katika majaribio ya watumiaji," anasema.

Mkurugenzi Mpulla anasema kuna mkakati na maandalizi yake yanafanyika ili kuwafikia walio mbali kwa maana migogoro itakayokuwa imesajiliwa kutoka maeneo ya mbali watairatibu na kuipangia tarehe kisha msuluhishi ama muamuzi wa migogoro atakwenda waliko.

"Mfano mwezi huu tumepokea kesi fulani kutoka wilaya moja, tutakwenda kuwajulisha siku tunayokuja lengo kuwapunguzia gharama tutawafuata waliko ... ni kurahisisha na kuwasogezea wananchi huduma karibu."

**UELEWA TATIZO**

Mpulla anaeleza kuwa moja ya changamoto zinazosababisha wafanyakazi wengi kupoteza haki zao ni uelewa mdogo katika kuwasilisha migogoro yao ndani ya muda uliowekwa kisheria.

"Wafanyakazi wanatakiwa kutambua changamoto kadhaa ambazo zinasababisha wengi kupoteza haki zao ni vyema wakazitambua. Mosi ni uelewa mdogo wa wafanyakazi wengi kujua ni wapi pa kuipeleka," anasema Mpulla.

INAENDELEA UK.13

ELIMU
NA BEATRICE PHILEMON

JANETH MAKWENJULA

# Atikisa Moro akiungana na Rais nishati safi jikoni



Janeth Makwenjula (kulia), akikabidhi mitungi ya gesi yenye jiko kwa wanawake wafanyabiashara migahawani. **PICHA: UWT**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ni championi wa nishati safi ya kupikia na ulinzi wa mazingira, aliye mstari wa mbele kuhimiza nishati safi jikoni ili kuboresha maisha ya Watanzania hasa kinamama.

Mbali na hilo ni kinara kuhimiza wananchi kuachana na nishati chafu kama vile mkaa, kuni, mafuta ya taa na kinyesi cha wanyama ambayo huleta athari za kiafya, kimazingira, kiuchumi na kijamii. Ni wazi kuwa Tanzania ni kubwa na inahitaji elimu ya jiko lisilochafua mazingira wala afya kumfikia kila mwanamama na umma pia, anasema Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT) Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro Janeth Makwenjula, anayeunga mkono matumizi ya nishati safi.

Anawafundisha na kuwahamasisha wanawake Wilaya ya Ulanga wakiwamo wajasiriamali, mama na babalishe na wafanyabiashara wenye migahawa kuanza kutumia gesi ya mitungi LPG.

Anasema hadi sasa amehamasisha kinamama wa kata zote 21 za Wilaya ya Ulanga jinsi ya kutumia jiko la gesi na pia kupanda miti katika maeneo yao.

"Hivi sasa mwamko wa matumizi ya majiko ya gesi katika kata ya Milola unaanza kuwa mkubwa wanawake wengi wanajitokeza kujifunza pia wanaume wamehamasika kuzinunulia familia zao majiko ya gesi..." anasema.

### MBINU ANAZOTUMIA

Janeth anasema amekuwa akitumia vikao vya umoja wa kinamama kuelimisha umma matumizi ya nishati safi vijijini, kata na wilaya.

Anasema anakusudia kuleta mabadiliko maana kwa sasa mahitaji ni mengi vijijini, wananchi wanazungumzia umuhimu wa mitungi lakini bei ipunguzwe kwa mitungi na gesi kwasababu wananchi wanategemea kilimo cha mpunga na hawana kipato cha uhakika.

"Baada ya kuona mwamko wa wanawake kuanza kuhitaji majiko ya gesi kuwa mkubwa, nimemuomba msaada mbunge wa viti maalumu mkoa, Christine Ishengoma, majiko ya gesi 67 ili niweze kufundishia wanawake na mengine kugawa kwa viongozi wa kata ili wanisaidie kuelimisha wanawake katika maeneo yao."

"Namshukuru sana Mama Ishengoma kwa sababu wakati wa kutoa elimu nilifanikiwa kugawa majiko ya gesi 12 kwa mamalishe katika kata ya Mahenge, majiko Milola na 50 kwenye kata zote 21 za wilaya ya Ulanga kwa wenyekiti na makatibu wa UWT wa kila kata kila moja ikipata majiko mawili," anasema.

Mbunge wa Ulanga, Salim Hasham, anamwongezea majiko 200 ya gesi kwa ajili ya kuendelea kuhamasisha kinamama kwenye vijiji, tarafa, kata mkoani humo kuhusu matumizi ya nishati safi.

"Nimegawa majiko haya katika kata ya Mahenge, Lupilo, Ruaha na Mwaya, lengo ni kuhamasisha wanawake kuacha kutumia kuni, mkaa na kutunza mazingira, zaidi ya wanawake 200 wamenufaika na msaada huu."

### MAZINGIRA BORA

Mbali na hilo, anahamasisha kinamama kuhifadhi wa mazingira na upandaji wa miti kwenye sehemu wanazoishi ili kuhifadhi mazingira, kuzuia mmomonyoko wa udongo hasa sehemu za milimani ambapo hivi sasa miti mingi imekatwa na wafugaji kwa ajili ya kilimo, kuchoma mkaa na kuni.

Hadi sasa wanawake wamepanda miti 52 katika kata ya Milola, miti 100 katika zahati ya Mavimba na mingine 1,000 katika kata ya Mahenge.

"Nimeamua kuanzisha kampeni hii baada ya kuona hali ya ukataji misitu katika wilaya ya Ulanga ni kubwa, wafugaji wanakata kupata malisho, kuni, kuchoma mkaa na shughuli za kilimo," anaelezea.

Pia athari za mazingira ni kubwa, hivi sasa msitu uliopo kwenye mlima wa Ndololo miti mingi imekatwa, wafugaji wanachoma mkaa ba eneo linaelekea kuwa jangwa, anasema.

"Wakati wa mafunzo niliwafundisha kinamama kupanda miti kwenye eneo la majumbani mwao, kwenye viwanja, mashamba yao ya kilimo kwa ajili ya kuzuia upepo na pia kwenye misitu na mashamba ya vijiji na kila kijiji kimepewa miche ya kupanda wanayopata kutoka Halmashauri ya wilaya ya Mahenge.

Pia hivi sasa wamepanda miche ya miembe 68 kwenye eneo la ekari mbili katika Kijiji cha Chikuti kilichopo jirani na Milola, anasema Janeth.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Kijiji cha Milola, Harun Mholoholo anakiri kuwa baadhi ya wananchi wameanza kutumia majiko ya gesi lakini bado ni wachache.

Anaomba serikali au wafanyabiashara wanaouza majiko ya gesi wasogeze huduma hii karibu na wananchi katika kata au au vijiji ili iwe rahisi kwa kinamama na wananchi wengine kupata majiko hayo kwa urahisi na kwa bei nafuu.

## Waajiriwa kupoteza haki nyingi kazini kumbe wanapofeli ni hapa

INATOKA UK.11

Aidha, anasema wengine wanaachishwa kazi wanakwenda kulalamika kwa Mkuu wa Mkoa ama Mkuu wa Wilaya na kujikuta akichelewa kupata haki zake kwa kuwa ameenda sehemu ambayo sio sahihi.

"Unaachishwa kazi unakwenda kulalamiko kwa mbunge, kwa waziri ama kwa mkuu wa mkoa kwa ufupi wanawasilisha malalamiko kwa wanasiasa kisheria hao hawana mamlaka wanapokwenda huko wanajichelewesha wenyewe na kujikuta wamepoteza haki zao kwa sababu sheria inaelekeza kesi ya kuachishwa kazi ifunguliwe kwenye CMA ndani ya siku 30," anakumbusha Mpulla.

Anaongeza: "Unamfuata mwanasiasa anamwambia anaweza kusema nisubiri au yupo bungeni au kwenye ziara halafu siku 30 zimekisha kwetu kesi inafutwa kwa sababu ipo nje ya muda."

Mpulla anasema hiyo ni moja ya changamoto kubwa wengi wanaopoteza haki zao kwa sababu ya kutokuwasilisha migogoro ndani ya wakati uliowekwa kisheria.

Anasema ukiachilia mbali kuachishwa kazi, migogoro mingine sheria inataka iwasilishwe ndani ya siku 60, hivyo hawapaswi kwenda sehemu yoyote bali kufika CMA.

### KUMALIZA KESI

Mpulla anasema mkakati wao wa kwanza ni kuhakikisha kesi ya usuluhishi inaisha ndani ya siku 30 tangu kufunguliwa muda uliopo kisheria.

Anasema mkakati wao wa ndani wamejiwekea siku 21 kwa kutambua umuhimu wao na endapo ikatokea usuluhishi ukashindikana katika uamuzi baada ya kusikiliza uamuzi unatakiwa utoke ndani ya siku 30 ambayo ni hukumu.

### KESI ZINAZOSAJILIWA

Akizungumzia idadi ya kesi wanazozipokea, Mpulla anasema inategemea na mwaka utakavyokuwa na kwa makadiri kwa mwaka kesi zaidi ya 10,000 zinasajiliwa CMA.

ELIMU

NA JALIWASON JASSON, MANYARA

# Viboko kwa watoto, wanafunzi adhabu inayozidi kulumbaniwa



Wadau wanapinga ukatili kama huu unaozidi adhabu. **PICHA: MTANDAO**

ADHABU ya viboko hutumika kuwakanya na kuwarudi watoto na wanafunzi shuleni. Ni kwa nadra walimu, wazazi au walezi wakaacha kiboko kwenye malezi.

Lakini ipo shuleni msingi na sekondari ili kuwaweka watoto au wanafunzi kwenye mstari darasani lakini pia suala la nidhamu kiboko hakiwezi kuwa mbali.

Gumzo la adhabu hii ni la siku nyingi na kila wakati linaibuka, mathalani wazazi na walezi wilayani Babati mkoani Manyara wana haya.

Musa Rehan, anaungana na kundi la wanaokubali adhabu ya viboko iendelee kwenye malezi na makuzi ili kurekebisha nidhamu ya mtoto au mwanafunzi.

Ana ushuhuda kuwa akiwa mwenyekiti wa kamati ya Shule ya Msingi Oysterbay iliyopo Babati mwaka 2005 alisimamia kiboko kidumu.

"Mtoto kuchapwa ni kukosolewa, kunyooshwa na kurekebishwa ambao hawachapwi ndiyo wanakuwa mateja, wavuta bangi na walevi."

Akiwa mwenyekiti wa kamati ya shule alipokea wajumbe wa tume ya kuangalia utoaji wa adhabu shuleni ambapo ilikuwa inataka mwalimu mkuu aruhusu kuchapa, aliigomea kwasababu mwalimu yeyote anachapa kwa nia ya kurekebisha na kujenga wala si kuumiza.

Rehan anasema watoto wasipochapwa ni kuwalea kizembe na kuongeza: "Sioni sababu mwalimu akitaka kumwadhibu mwanafunzi aombe ruhusa kwa mwalimu mkuu, yote haya yanaleta kudharauliwa na wanafunzi," anaonya Rehan.

Mkazi wa Mtaa wa Komoto, John Tango, anaungana na Rehen akisema hakuna tatizo bali walimu wanaochapa kupita kiasi hata kuumiza wanakosea.

Tango anasema watoto hata nyumbani wazazi na walezi wanawaadhibu ila kwa kiwango cha chini kisichokuwa na madhara kiafya na kisaikolojia.

Mkazi wa Kijiji cha Bermi Adelina Paul, anaipinga kwa maelezo kuwa inasababisha baadhi ya wanafunzi kuikataa shule.

"Ukifatilia wengi walioacha shule chanzo ni kiboko," anasema Adelina na kushauri iwepo sheria ya kuadhibu wanaochapa kiboko kupita kiasi, iwahusu walimu au wazazi.

Mkazi mwingine wa Kijiji cha Matufa Halima Halfan anasema adhabu ya viboko inawaumiza wanafunzi kuwajengea woga na kusababisha washindwe kujiamini.

## KUISHIWA MBINU

Meneja mradi na elimu wa Shirika la So They Can (STC), Grace Swai, anasema viboko vimepitwa na wakati na anayetumia adhabu hiyo ameishiwa mbinu.

"Ukimchapa mwanafunzi unamweka mbali na wewe ili asijifunze zaidi. Wapo watoto wanalea familia, wanatoka mbali na shule ila walimu hawawasikilizi anawaadhibu," anasema Grace.

Anataja sheria ya elimu ya mwaka 1978, inayoagiza kuwa mwalimu mkuu ndiye anatakiwa kutoa ruhusa ya kuchapa viboko tena kwa maandishi.

Grace anatahadharisha walimu na kutumia viboko kuwa watoto wengine wakichapwa wanazimia au kupoteza maisha hivyo wawe makini au waiepuke adhabu hiyo.

Ofisa Mradi wa Sauti Yangu, wa Shirika la So They Can, Peter Nelson, anasema mradi wao unawajengea uwezo wanafunzi kujua haki zao, kusema vitu wanavyovipenda au wasivyovipenda vinavyofanywa na walimu shuleni.

Nelson anasema wamewafikia wanafunzi wa shule za msingi kuanzia darasa la awali mpaka darasa la saba 17,000 na wa sekondari 21,000.

Aidha, anasema walimu zaidi ya 300 wamewapatia elimu ya mbinu za kuepuka kutoa adhabu ya viboko.

Licha ya mbinu hiyo anasema walimu wanatembelea shule za mchepuo wa Kingereza kujifunza namna ya kutoa adhabu bila kutumia viboko akitoa mfano kuwa mwanafunzi anaweza kupewa kadi, kunyimwa ruhusa ya kucheza na wenzake.

Ofisa huyo anasema kabla ya STC kuanza kutoa elimu kwa walimu shule nyingi walikuwa wakiwapiga viboko lakini kwa sasa mambo yamebadilika.

Anaongeza kuwa awali walimu wa kiume walikuwa wanawachapa wanafunzi wa kike viboko kwenye makalio licha ya kwamba ni kinyume na utaratibu.

Nelson anasema serikali iendelee kutoa mafunzo vyuo vya ualimu na walimu waondoe fikra mgando za ya kuendeleza viboko.

Mkuu wa Programu, Godfrey Bonaventure, kutoka Shirika la HakiElimu anasema hali halisi ya matumizi ya viboko na uzoefu wa kutokuvitumia inaonyesha wengi wamezoea kuchapwa.

Anafafanua kuwa asilimia 87.9 ya watoto shuleni wamezoea kuchapwa na asilimia 90 wanapigwa, akiuita ukatili waliouzoea.

Boniventure anasema utafiti wa HakiElimu unaonyesha kuwa asilimia 89.0 wamezoea kuchapwa shuleni, wakati 10 wamezoea kuchapwa nyumbani akisema asilimia 37.1 wanachapwa na ni aina ya adhabu inayotumiwa na walimu kila siku vijijini.

Anaongeza kuwa asilimia 16.3 ni aina ya adhabu inayotumiwa na walimu mijini kila siku.

Utafiti huo unaonyesha mataifa ya Afrika yanayochapa viboko ndani ya miezi 12 ikiwamo Tanzania yenye asilimia 43.

Uganda 35, Malawi 25, Kenya 21, Nigeria 19, Zambia tisa, Lethoto nne na Zimbabwe nne.

Katika utafiti huo wanafunzi wanasema: "Nikichapwa viboko napata maumivu makali yananifanya nisiwe na utulivu darasani. Yaani sitamwelewa mwalimu kabisa"

"Viboko vinatufanya tuwaogope walimu na kushindwa kuomba msaada unapohitajika" "Siwapendi walimu wanaotumia viboko."

## ADHABU CHANYA

Utafiti huo umezungumzia adhabu chanya kuwa adhabu kali ilikuwa asilimia mbili, kazi za ziada za mtaala asilimia 18, kazi za shuleni kufanyia nyumbani asilimia 10, kumwongoza na kumshauri asilimia 26 na kusafisha madarasa asilimia 44.

Taarifa ya Mtandao wa Elimu Tanzania(TENMET), ya Septemba 2018 ililaani adhabu ya viboko.

TENMET inawakumbusha walimu na wananchi kuwa muongozo wa kutoa adhabu mashuleni chini ya kifungu cha 61(1)(v) cha sheria ya elimu sura ya 353 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 inaeleekza utoaji wa adhabu hiyo.

TENMET inasema mtoto ana haki ya kulindwa, kuendelezwa, kuishi, kushirikishwa na kutobaguliwa.

Mshauri wa malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto Davis Gisuka kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC), anasema walimu wanaotoa adhabu ya viboko kwa wanafunzi wa chekechea wanawaharibu makuzi ya ubongo.

Gisuka anasema wakiwa wanachapwa viboko akili yao itakuwa chini na hata wakienda shule hawataweza kujifunza vizuri na kuelewa.

Aliyataja madhara wanayoweza kuyapata wanafunzi wa chekechea kuwa ni wanafunzi wote kuumia, kuharibika kisaikolojia na kuwajengea woga.

Vile vile anasema walimu wanaocharaza bakora wanaharibu mahusiano yao na wanafunzi na wengine kuwafanya wachukie shule.

> Ukimchapa mwanafunzi unamweka mbali na wewe ili asijifunze zaidi. Wapo watoto wanalea familia, wanatoka mbali na shule ila walimu hawawasikilizi anawaadhibu.

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Mkono wa Taasisi Elimu ya Juu kuboresha afya ulipoikuna WHO

JUHUDI za kuboresha huduma za afya ya Mtanzania zinazofanywa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), zimeligusa Shirika la Afya Duniani (WHO) linalotangaza kuzitambua na kuziendeleza.

Utambuzi huo unakihusisha pia Chuo Kikuu Mzumbe pamoja na mashirika mengine 11 ya kitaifa na kimataifa yanayofanya juhudi za kuboresha afya ya Mtanzania, kwa kugusa mifumo ya kutoa huduma hizo.

Katika kuendeleza juhudi hizo, WHO inaingia makubaliano na taasisi hizo na kuafikiana kufanyakazi zaidi na kuleta mapinduzi ya kumpa afya bora kila mwananchi.

Mkuu wa Chuo cha DUCE, Profesa Stephen Maluka, akizungumza na Nipashe, baada ya kusaini makubaliano na WHO, jijini Dar es Salaam hivi karibuni anasema moja ya mambo yaliyofanywa na taasisi hiyo ni utafiti wa uwajibikaji wa vyombo vya kusimamia utoaji huduma za afya.

Itakumbukwa kuwa mwaka 2022 katika mradi wa kutathmini uwajibikaji wa kamati za usimamizi wa vituo vya afya na bodi za afya za halmashauri ulifanyika utafiti katika wilaya za Mbarali mkoani Mbeya na Handeni Tanga na kubainika kuwa kulikuwa na kukosekana uwajibikaji, anasema Profesa Stephen Maluka.

Akizungumza na Nipashe baada ya kutambuliwa na WHO, Profesa Stephen Maluka, anasema ushiriki wa chuo kwenye tafiti mbalimbali umekipa heshima hiyo na kukifikisha kwenye hatua hiyo ya kujivunia.

Anaongeza kuwa DUCE inaratibu mradi wa miaka mitatu ulioanza 2021 hadi 2024 unatarajia kuongeza uwajibikaji wa kamati za usimamizi wa vituo vya afya na bodi za afya za halmashauri.

Anakumbusha kuwa awali utafiti huo uliozihusisha wilaya za Mbarali na Mji wa Handeni ukiwashirikisha wananchi 1,184 na kubaini kuwa asilimia kubwa ya wananchi hawajui iwapo kuna kamati za usimamizi wa vituo vya afya pamoja na bodi za afya za halmashauri, ambazo zipo kwa ajili ya kusimamia utoaji wa huduma kwenye vituo na hospitali za wilaya.

Profesa Maluka, akiwa mtafiti kiongozi anasema: "Utafiti huo ulilenga mambo mawili makubwa, kutathmini uelewa wa wananchi kuhusu utendaji kazi wa kamati za usimamizi wa vituo vya afya. Pamoja na kutathmini uwajibikaji wa kamati za usimamizi wa vituo vya afya na bodi za afya za halmashauri."




Viongozi wa taasisi zilizotambuliwa na WHO kuboresha afya. **PICHA: WHO**

> Asilimia 85.3 ya wananchi walikuwa hawajui kama kuna kamati hizo wakati asilimia 96.5 walikuwa hawana habari za uwepo wa bodi za afya za hospitali za halmashauri.

Anasema katika kuleta mabadiliko na kuongeza uelewa miongoni mwa jamii, matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa wadau kuanzia wananchi, wajumbe wa kamati, bodi, watendaji wa serikali kama vile waganga wakuu wa wilaya hizo na wakurugenzi.

"Asilimia 85.3 ya wananchi walikuwa hawajui kama kuna kamati hizo wakati asilimia 96.5 walikuwa hawana habari za uwepo wa bodi za afya za hospitali za halmashauri."

Aidha anasema asilimia 88.3 ya wananchi waliohusishwa walibainika kuwa hawakuwahi kusikia kuhusu uchaguzi wa wajumbe wala kushiriki kuwachagua wajumbe wa kamati na bodi hizo ili kusimamia huduma.

"Kama wananchi hawajui kuna kamati za usimamizi maana yake hata uwajibikaji wa hizi kamati na bodi ni changamoto." Anaeleza.

Kutokana na uelewa wa wananchi kuwa mdogo, Profesa Maluka anasema pia utafiti ulionesha asilimia 96.7 hawajawahi kupata mrejesho wowote kutoka kwenye vyombo hivyo vya usimamizi na kudhihirisha kuwa uhusiano kati ya kamati, bodi na wananchi ni mdogo.

Baada ya matokeo hayo, watafiti walitoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kuwafikia wananchi kuhusu majukumu na utendaji kazi za kusimamia vituo na hospitali ili kuongeza uelewa na uwajibikaji wa mamlaka hizo za usimamizi. Aidha, anasema lengo ni kuimarishwa, ili zisiwajibike kikamilifu kwa watu na kusimamia fedha zinazowekezwa kwenye vituo vya afya na hospitali za wilaya kote nchini.

Akizungumzia makubaliano na WHO, anaeleza kuwa yatafanikisha utoaji wa elimu kwa wananchi na wadau wa afya, kuboresha elimu ya lishe, mifumo ya utoaji huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto pamoja na kinga, kadhalika kutekeleza vipaumbele vya serikali," anasema Profesa Maluka.

Profesa Peter Kamuzora, kutoka Taasisi ya Taaluma za Maendeleo UDSM, anasema hatua ya mabadiliko kwenye sekta ya afya imewezesha wananchi kushirikishwa katika mipango ya kiafya ya mwaka na kutoa maamuzi katika huduma.

Anasema hilo linafanyika kupitia wawakilishi wao kwenye kamati za usimamizi wa vituo vya afya ngazi ya zahanati, kituo cha afya na hospitali na bodi za huduma za afya za halmashauri.

Profesa Kamuzora, anataja hayo anapowasilisha mada kuhusu chimbuko na mabadiliko kwenye sekta ya afya nchini, kwenye mafunzo ya siku mbili yaliyohusisha wajumbe, wenyeviti, makatibu wa bodi na kamati hizo pamoja na maofisa watendaji kata wa wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya.

"Matokeo na maendeleo katika utekelezaji wa mabadiliko katika sekta ya afya, wizara inaendelea kushughulikia uanzishwaji wa bima ya afya kwa wote, aidha inaendelea kushirikisha sekta binafsi na wadau wote katika kuimarisha huduma hizo," anafafanua.

Anaongeza: "Serikali imezifanyia mapitio sheria mbalimbali na kuanzisha nyingine, mfano, sheria ya bima ya afya ya taifa (1999) na sheria ya mfuko wa afya ya jamii (2001), pia imebuni vyanzo vingine vya mapato, ili kugharamia huduma za afya papo kwa papo..."

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la WHO, Dk. Charles Sagoe-Moses, anasifu wadau wote, akisema kuwa makubaliano na taasisi hizo yametambua mchango mkubwa unaofanywa na mashirika mbalimbali kwenye sekta ya afya, kuhakikisha hakuna anayeachwa kando.

"WHO inatambua thamani na kinachofanywa na taasisi hizi, kuboresha huduma za afya, hususan kwenye ajenda ya afya kwa wote," anasema Dk. Charles na kwamba makubaliano hayo yatajikita katika kuimarisha mifumo ya afya, kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza (NCDs), ya mlipuko na kuhimiza mtindo bora maisha.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACONGo), Rachel Chagonja, akiweka saini pamoja na WHO, kwa niaba ya mashirika 11, anasema makubaliano hayo yanabainisha nia ya kuongeza wigo wa huduma zinazomfikia kila Mtanzania.

Anafafanua kwamba, makubaliano yanawiana na ya shirika hilo, kwenye sekta ya afya, kwa kuwajengea uwezo wataalamu, kufanya utafiti na kuimarisha mifumo, huduma za afya ngazi ya jamii.

Katika utambuzi huo pamoja na DUCE, Shirika la Afya Duniani pia limevitambua vyuo na taasisi kadhaa zikiwamo Taasisi ya Catholic Relief Services (CRS), Doctors with Africa (CUAMM), SIKIKA, Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania Health Summit (THS) na AMREF HEALTH AFRICA Tanzania.

Wengine ni International Rescue Committee, Ifakara Health Institute (IHI), Raising Up Friendship Foundation (RUFFO) pamoja na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).



# Bil.71/- zatumika sekta ya afya miaka mitatu ya Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. bilioni 71.9 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya mkoani hapa.

Amesema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 34.5 zimetumika kuboresha miundombinu ya afya na Sh. bilioni 37.2 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba, mashine na vitendanishi.

Alisema hayo baada ya kukabidhiwa msaada wa vifaa vya mbaliimbali vya huduma za kiafya vilivyotolewa kwa ajili ya afya ya uzazi na mtoto kutoka Shirika la Italiani (AICS).

Alisema kuwa msaada huo wa vifaa vya afya utafanikisha kwa sehemu kubwa kuboresha huduma kwa wananchi kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali.

Senyamule alisema vifaa hivyo vilivyotolewa kutoka Serikali ya Italia inaonyesha ni jinsi gani wanavyounga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea kuboresha huduma za afya nchini.

Aidha, aliwataka wananchi wa mkoa wa huo kutumia fursa hiyo kupata huduma katika vituo vilivyo karibu, huku akiwasisitizia wajawazito kuhakikisha wanahudhuria kliniki kwa wakati.

**Amesema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 34.5 zimetumika kuboresha miundombinu ya afya na Sh. bilioni 37.2 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba, mashine na vitendanishi.**

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la AICS Tanzania, Paolo Razzini, alisema wanatekeleza mradi wa kuboresha huduma za afya ya uzazi kwa kipindi cha miaka miwili ambao utakamilika Juni 2025.

Alisema kuwa mradi huo unatekelezwa kwa Sh. bilioni 1.8 ambazo zitatumika kwa manunuzi ya vifaa tiba na mafunzo ya kuwajengea uwezo kwa watoa huduma.

Kaimu Mkurugenzi wa Shirika CMSR, Dk. Hamud Ndenge, alisema kuwa vifaa vya afya wanalivyokabidhi vimegharimu Sh. milioni 483.7.

Alisema vifaa hivyo vitapelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma ikiwamo Makole, Mkonze, Hombolo na St. Gema lengo ni kuunga mkono jitihada za Rais Samia kuboresha huduma za afya.

"Tunakabidhi vifaa hivi vitakavyotumika katika kuboresha huduma za afya lengo ni kuendelea kuunga mkono jitihada za Rais Samia za kupunguza vifo vya mama na mtoto na kufikia lengo," alisema.

Hata hivyo, alisema vifaa hivyo pia vitasaidia kuongeza upatikanaji wa huduma bora za dharura kutoa mafunzo kwa watoa huduma na kuboresha huduma za upasuaji kwa wajawazito.




Kaimu Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitalli ya Makole, Frola Mwakalobo (wa pili kulia), akipokea mashine moja ya vifaa vya afya ya uzazi na mtoto kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rose Senyamule, vilivyotolewa kwa ufadhili na Shirika la Italia (AICS) vyenye gharama ya Sh. bilioni 71.9 katika makabidhiano yaliyofanyika hospitali hapo jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la (AICA), Paolo Razzini. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Jeshi laonya wanaotapeli, kuuza nafasi za mafunzo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limesema litawachukulia hatua kali za kisheria, ikiwamo kuwapa adhabu baadhi ya watu watakaobainika kufanya utapeli wa kuuza nafasi za vijana wanaojiunga na mafunzo ya jeshi hilo kwa mujibu wa sheria.

Pia, limewataka vijana walioahitimu kidato cha sita kuripoti katika kambi mbalimbali za jeshi hilo kuanzia Juni Mosi hadi 7 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa, Mkuu wa Tawi la Utawala wa JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena alisema mafunzo hayo hutolewa bure lakini kuna watu wamekuwa wakitumia kutapeli raia wenye uhitaji wa mafunzo hayo.

Alisema serikali imekuwa ikitenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya shughuli za JKT ikiwamo kuboresha mafunzo ya vijana na miundombinu, hivyo hakuna mtu yeyote anayeruhusiwa kuuza nafasi kwa vijana hao.

"Jeshi halitakuwa na huruma kwa mtu yeyote atakayebainika kufanya kitendo hicho na kusisitiza wananchi wasirubunike, badala yake waingie kwenye tovuti ya JKT watapata taarifa zote," alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Alisema wazazi wenye watoto wanaotaka kujiunga na JKT wamekuwa wakitapeliwa fedha na kutapeli gharama kubwa ya kuandaa vifaa vinavyohitajika wanapokuwa mafunzoni kitu ambacho siyo sahihi.

Brigedia Jenerali Mabena alisema vitendo hivyo vinafanywa na watu wenye nia ovu jambo ambalo halikubaliki, kwamba jeshi haliuzi nafasi hizo wala halifanyi biashara yeyote.

Brigedia Jeneral Mabena alisema jeshi limewapangia vijana makambi watakayokwenda kupatiwa mafunzo na wanatakiwa kuripoti kuanzia Juni Mosi.

Kuhusu maandalizi, alisema JKT imekamilisha, wakufunzi wameendelea kupatiwa mafunzo na semina elekezi namna ya kuwafunza vijana hao watakapowasili.

# Kamati yasisitiza uzalishaji madaraja ya vyuma nchini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeitaka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kwa kushirikiana na taasisi nyingine kuangalia uwezekano wa kuzalisha madaraja ya vyuma nchini badala ya kuagiza kutoka nje.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Denis Londo, alitoa agizo juzi baada ya wabunge wa kamati hiyo kutembelea daraja la vyuma la Mto Minyughe lililopo wilayani Ikungi mkoani Singida.

Ujenzi wa daraja hilo umegharimu Sh.bilioni 1.815 ambazo kati ya hizo Sh. bilioni 1.259 zilitumika kununulia vyuma vya daraja hilo kutoka nje ya nchi.

"Ni wakati sasa wa kuangalia teknolojia ile ya madaraja ya vyuma tukaanza kuzalisha hapa nchini wenyewe kwa kutumia mahusiano yetu kati ya nchi na nchi badala ya kuendelea kuagiza nje tena kwa fedha za kigeni ambazo bado tuna changamoto nazo," alisema.

Aidha, Londo aliitaka TARURA suala la ujenzi wa mifereji katika barabara zinazojengwa iwe ajenda ya kudumu kwa nchi nzima, vinginevyo serikali itakuwa inawekeza fedha katika ujenzi wa barabara ambazo hazitadumu kwa muda mrefu.

Naye Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seif, alisema Daraja la Minyughe wananchi kwa serikali wasaidie kulilinda lisiweze kuhujumiwa kwa kuibiwa vyuma na kwamba wakala ilishatoa maelekezo kwa mameneja wa mikoa na wilaya kila barabara zinapojengwa ziwe zinawekwa taa.

Alisema TARURA imeshafanya utafiti na kubaini kwamba kunahitajika taa 46,000 katika barabara zote zilizojengwa.

Nao baadhi ya wabunge walisisitiza suala la kulilinda daraja hilo vyuma visiweze kuibiwa kwa kuweka taa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa daraja na kwamba mitaro ijengwe.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Ibrahim Kibasa, alisema Daraja la Minyughe (mita 30) ambalo lilikatika na kusababisha kukosekana kwa mawasiliano kwa wananchi wa kata za Maklawa na Minyughe, ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 98 na hadi sasa zimetumika Sh. bilioni 1.815.





# Waziri ataja faida cheti cha kuzaliwa

**Ibrahimu Joseph na Elizabeth John**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana, amewataka wazazi na walezi kuwachukulia watoto wao vyeti vya kuzaliwa, ili viweze kuwasaidia wakati wa baadaye.

Alitoa wito huo juzi baada ya kutembelea mabanda kwenye kampeni ya msaada wa kisheria mkoani hapa.

Alisema kuwa wazazi na walezi wanatakiwa kuwachukulia watoto wao vyeti vya kuzaliwa kwa ajili ya kuwasaidia kuvitumia kwenye maisha yao ya baadaye.

"Kwa kweli cheti cha kuzaliwa ni muhimu na kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu mtoto yeyote anayezaliwa Tanzania anayo haki ya kupata cheti," alisema Dk. Chana.

Aliyataja manufaa ya kupata vyeti vya kuzaliwa kuwa ni pamoja na kusaidia kupata Kitambulisho cha Utaifa, mikopo ya elimu ya juu na hati za kusafiria.

Alisema endapo wazazi na walezi watachukukuwa vyeti vya kuzaliwa itaisaidia serikali kupata takwimu kwa ajili ya mipango ya baadaye ya maendeleo.

**"Mimi eneo langu limevamiwa na watu, nimekuja hapa kupata ushauri kwa sababu amri ya mahakama ilitolewa kwamba waondoke lakini wao hawataki kutoka," alisema Tweve.**

Aidha, alisema kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inatakiwa kuendelea kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani, lengo likiwa ni kuwafikia wananchi wanyonge wasiokuwa na uwezo wa kuwalipa mawakili kwa ajili ya kupata haki.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini aliwataka wananchi kujitokeza ili kupata ushauri wa kitaalamu kuhusu mirathi, migogoro ya ndoa na ardhi.

"Migogoro hii imekuwa ikisababisha mfarakano kwenye familia na jamii au wakati mwingine kuleta madhara kwa sababu tunaweza kumaliza migogoro kwa njia ya kistaarabu," alisema Sagini.

Alisema kuwa kuna mambo ya kupewa ushauri kama kuna wengine wanamigogoro na watoto wao wanadaiana ardhi wanataka kurithi kabla hawajafa.

Mmoja wa wananchi akiwamo, Simon Tweve alisema kampeni hiyo imekuja wakati sahihi kwa sababu kuna migogoro ya muda mrefu ambayo ilishindwa kupatiwa ufumbuzi.

"Mimi eneo langu limevamiwa na watu, nimekuja hapa kupata ushauri kwa sababu amri ya mahakama ilitolewa kwamba waondoke lakini wao hawataki kutoka," alisema Tweve.

Naye Mary Sanga aliishukuru serikali kwa kuleta msaada wa kisheria kwa sababu kuna gharama kubwa ya kuwapata mawakili.




Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini (kulia), akimsikiliza Mkazi wa Mjimwema Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe, Casian Njarika (80), alipofika kwenye banda la wizara hiyo kupata huduma ya msaada wa kisheria wa Mama Samia jana inayoendelea mkoani hapo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# W'biashara Tanzania watakiwa kuwavuta wenzao nchi jirani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeitaka Chemba ya Wafanyabiashara na Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), kuwashawishi wafanyabiashara wa nchi jirani, zikiwamo za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), washiriki kwenye maonyesho ya biashara (Mbeya City Expo) ili kubadilishana uzoefu.

Mataifa hayo ni Malawi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambayo yako jirani na mabalozi wa nchi hizo wamekuwa wakialikwa kushiriki kwenye maonyesho hayo.

Akizungumza wakati wa kufungua maonesho kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kufanya hivyo kutasaidia kuziona bidhaa mbalimbali na kujifunza jinsi ambavyo wafanyabiashara wa mataifa mengine wanavyoandaa na kudumisha ubora wa bidhaa zao.

Alisema faida nyingine ya kuja kwa wafanyabiashara kutoka kwenye mataifa hayo ni kutengeneza mfumo ambao utawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kwenda kwenye nchi hizo kuonesha bidhaa zao na kutatanua wigo wa soko utakaoboresha kipato chao na pato la taifa.

Homera aliwataka wadau wa biashara kuzitumia fursa zilizopo Mkoa wa Mbeya ikiwemo miundombinu ya usafiri majini upande wa Ziwa Nyasa, usafiri wa anga na Uwanja wa Ndege wa Kitaimafa Songwe.

"Hivi sasa zinafanyika safari za usiku, barabara ya njia nne imeanza kujengwa sambamba na reli ya TAZARA ambayo serikali imepanga kuiboresha ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kuja kwenye mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na nchi jirani za Malawi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, hivyo tunatakiwa kuwashirikisha," alisema Homera.

Rais wa TCCIA, Vicent Minja, alisema kuwa miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kumekuwa na mabadiliko makubwa katika sekta ya uwekezaji na uchumi ambapo kituo cha uwekezaji kimerekodi miradi mipya zaidi ya 1,188 ambalo ni ongezeko la asilimia 63.19 ikilinganishwa na miaka mitatu iliyopita.

Minja alisema kasi ya serikali inaifanya TCCIA kuongeza kasi ya uboreshaji wa huduma katika sekta hizo ili kufikia malengo ya pamoja kwa ajili ya kuimarisha uwekezaji na uchumi nchini.

Mkurugenzi Msaidizi wa Maendeleo ya Biashara kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara Crestencia Mwimbwa, alitoa wito kwa wadau wanaoshiriki maonesho ya Mbeya City Expro 2024 kujifunza kuhusu biashara zinazopatikana katika maonesho na kuzitumia vyema fursa adhimu za tukio hilo.

Maonesho hayo mwaka huu ni ya pili kufanyika tangu yalipoanzishwa mwaka 2023 yakiwa ni maono ya TCCIA na Serikali ya Mkoa wa Mbeya na kuyafanya kuwa maonesho makubwa ya kimataifa kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

## Maofisa forodha, mazingira wapigwa msasa kudhibiti zebaki

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

MAOFISA wa forodha na mazingira wa mikoa ya Mbeya na Songwe, wamepewa mafunzo maalumu ya kuwawezesha kudhibiti kemikali aina ya zebaki.

Mafunzo hayo yalitolewa mwishoni mwa wiki na maofisa wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

Mafunzo hayo yalitolewa katika ofisi ya forodha iliyopo katika mpaka wa Tunduma ambapo ni miongoni mwa mipaka ya Tanzania na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Ofisa Mazingira wa NEMC, Boniface Kyaruzi alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uelewa wa namna sahihi ya usimamizi, uingizaji halali na matumizi salama ya kemikali ya zebaki kwa wachimbaji wadogo, ili kuepuka athari za kiafya na kimazingira.

Kyaruzi aliongeza kuwa mafunzo haya yanayoendeshwa kupitia Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Kemikali ya Zebaki (EHPMP) unaofadhiliwa na Benki Kuu ya Dunia (WB) na kuratibiwa na (NEMC) ni mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa maazimio ya mkataba wa MINAMATA.

"Moja ya matakwa ya mkataba ni kila nchi mwanachama kuandaa mpango kazi wa kitaifa wa namna sahihi ya kudhibiti matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo kwa dhumuni la kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa hiyo sisi kama taifa lazima tutekeleze," alisema Kyaruzi.

Naye Jansen Bilaro, ambaye ni mkemia kutoka Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Mkoa wa Mbeya, aliwataka maofisa hao kushirikiana bega kwa bega na Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Aliwataka kuhakikisha wanadhibiti uingizaji haramu na matumizi yasiyo salama ya kemikali ya zebaki kwa kuhakikisha waingizaji, wasambazaji na wachimbaji wadogo wanasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kemikali Namba Tatu ya Mwaka 2003 inayohusu usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani ikiwamo zebaki.



# Vijana wajuzi wa TEHAMA wanahitajika Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, amesema Zanzibar hivi sasa inahitaji vijana wenye taaluma ya masuala ya Sayansi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuendana na wakati wa sasa.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya TEHAMA kwa wanafunzi wa Shule ya Maarif, yaliyoandaliwa kwa ushirikiano wa shule hiyo na Shirika la Redio na Televisheni ya Uturuki (TRT).

Alisema ni vyema watoto kujengewa uwezo tangu wakiwa wadogo shuleni kutumia teknolojia ambayo itatoa uwezo wa kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo ubunifu.

Alisema mafunzo ya kidijitali kwa wanafunzi yatasaidia katika kuendelea na elimu yao na hata katika shughuli zao ambazo watakuja kuzifanya baada ya kumaliza masomo.

Alisema kuna vijana wengi wanafanya kazi za ubunifu, wanajua vitu lakini namna ya kutumia teknolojia ili kubuni vitu inakuwa ni ngumu, hivyo kupitia elimu hiyo itawasaidia kuwa wabunifu.

"Ulimwengu wa sasa ni wa teknolojia na umuhimu wake mkubwa ni kuhakikisha watakuwa na uwezo wa kutumia teknolojia katika shughuli zao mbalimbali," alisema Mgeni.

Hata hivyo alisema kwamba hivi sasa vijana wengi wakitumia simu za mkononi ambazo zinawasaidia kutafuta taarifa mbalimbali za masomo yao na mambo mengine ya kiujuzi, ambayo wanaweza kujifunza katika simu.

Alisema kupitia mafunzo hayo itawapa uwezo zaidi wa kuingia katika mitandao ili kuwasaidia kupata elimu ya ziada na kujua ulimwengu unavyokwenda kwa manufaa yao na taifa.

Mkufunzi wa mafunzo hayo kutoka TRT ya Uturuki, Alpay Ari, alisema kuwa wakitembea kila nchi kutoa elimu hiyo ya TEHAMA ili elimu hiyo iwafikie watu wengi kwa kuwa uandishi wa kidijitali ni muhimu katika ulimwengu wa sasa.

Alisema lengo la kutoa mafunzo hayo kwa wanafunzi wa shule hiyo ni vijana kujiandaa kwa ajili ya uandishi wa baadaye katika kutoa taarifa zenye manufaa katika jamii na nchi kwa ujumla.

"Katika mafunzo haya miongoni mwa tunayowafundisha ni jinsi ya uandaaji wa vipindi, habari na kupitia matukio mbalimbali ya kihabari," alisema.

Wanafunzi wa sayansi wa shule hiyo waliopatiwa mafunzo hayo akiwemo, Neel Sanjoy Roja na Rabia Suleiman Yahya walisema kuwa mafunzo hayo yatawasaidia namna ya kutumia teknolojia na kujua zaidi namna ya kutumia vifaa vya kidijitali pamoja na namna ya kuchukuwa habari tofauti zinazotokea katika jamii na kuhabarisha umma.

# Tathmini ongezeko wagumba Zanzibar bado haijafanyika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema hadi sasa haijafanya tathmini ya kina kuhusu ongezeko la tatizo la ugumba visiwani hapa.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh, alisema kwa mujibu wa taarifa zilizokusanywa kupitia mfumo wa taarifa za afya wa wizara inaonesha kuwa tatizo hilo lipo kwa wanawake na wanaume.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah aliyetaka kujua Wizara ya Afya imeshafanya tathmini yoyote kuhusiana na ongezeko la tatizo la ugumba visiwani Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kwa upande wa wanawake tatizo hilo limeonekana kusababishwa na maambukizi katika via vya uzazi, ukosefu wa vichocheo vya uzazi, msongo wa mawazo na uvimbe katika fuko la uzazi.

**Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh, alisema kwa mujibu wa taarifa zilizokusanywa kupitia mfumo wa taarifa za afya wa wizara inaonesha kuwa tatizo hilo lipo kwa wanawake na wanaume.**

"Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wanaume tatizo hili linasababishwa na uzalishaji hafifu wa mbegu za uzazi, mwonekano wa mbegu usio wa kawaida, msongo wa mawazo, tatizo la kimaumbile linalotokana na vinasaba," alisema.

Pia alisema ili kukabiliana na tatizo hilo wananchi wanatakiwa kubadilisha utaratibu wa lishe kwa kutumia vyakula vya asili, kutibiwa maradhi ya kujamiiana mapema, kufanya mazoezi, kuwachunguza watoto ili kugundua baadhi ya matatizo mapema na kuepuka matumizi ya sigara.

Aidha, alisema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau inaandaa miongozo ya kuwafuatilia watoto wenye umri wa zaidi ya miaka mitano mpaka kufikia balehe ili kuweza kuwafuatillia afya zao na kuwaandaa wawe na afya nzuri na kuwa wazazi wenye afya bora.



Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea Chukani nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Hakuna utafiti wa ongezeko la rushwa, uhujumu uchumi'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman amesema hakuna utafiti rasmi uliofanywa hivi karibuni na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) unaonesha ongezeko la moja kwa moja la vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah aliyetaka kujua tathmini ya ongezeko la vitendo vya rushwa visiwani Zanzibar ikoje kwa sasa.

Akijibu swali hilo, alisema taarifa za vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi zilizokusanywa na mamlaka kwa mwaka 2023 zinaonesha kwamba vitendo hivyo vimeongezeka kutoka 410 mwaka 2022 hadi 597 mwaka 2023.

Alisema ongezeko hilo linachangiwa kwa kiasi kikubwa uelewa na mwamko wa wananchi wa kuripoti vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi kupitia njia tofauti za utoaji taarifa.

Hata hivyo, alisema Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi inaendelea na juhudi za kutoa elimu kwa wananchi, kuimarisha miundombinu na mifumo ya uchunguzi.

"Pia mamlaka inaendelea kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba, vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi vinapungua zaidi licha ya kuwepo kwa mwamko mkubwa wa wananchi wa kuripoti vitendo hivyo," alisema.

Katika swali lingine, mwakilishi huyo pia alitaka kujua tathmini juu ya ongezeko la vijana wanaotumia dawa za kulevya kupitia vijijini hususani kwenye ukanda wa sekta za hoteli za kitalii Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman alisema, ofisi yake bado haijafanya tathmini hiyo kwa vijana lakini moja kati ya vipaumbele vya wizara kwa mwaka wa fedha 2024 ni kufanya tathmini juu ya matumizi ya dawa za kulevya kwa maeneo ya ukanda wa utalii Zanzibar.

Alisema katika Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2022 ambayo imewasilishwa katika Baraza la Wawakilishi imeonesha hali halisi ya makundi mbalimbali ya wananchi wakiwamo vijana wanaotumia dawa za kulevya ambao wanatumia aina tofauti za dawa hizo zikiwamo bangi, cocaine, heroin, mirungi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALOME MARKO MASANGU MTWEVE,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index no **S0801-0022-2003** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari Matora Mwaka 2003, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/20127/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MARCUS UPUGE NZWARILA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 425 CTJ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PHQ/IRI/MUF/4244/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IBRAHIM JIARRY SANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 600 CCT.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **GEI/GEI/RB/42922/2023**

## KUPOTELEWA NA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**ZACHARIA JULIUS BULUGU** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya Umiliki wa kiwanja namba 18 Kitalu "HH" kilichopo Ndala Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi Kilichopo karibu au awasiliane na Julius kwa simu namba **0786-488712**

TAARIFA YA POLISI: **PHQ/SHI/SHI/3180/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RASIK GOHIL** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye majina **Tanzania china Trade&tourism development,** namba za usajili **MC996AUG** aina ya **BOXER,** Chassis No. **LDAPAJOB2FGBC2815,** Engine No. **157FMI215F02815.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/513/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCAS SHAURI PALLANGYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 929 CVZ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/69183/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GUTA

**ABEL KUDALIKO SANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya guta yenye usajili namba **MC 991 EFQ.** Kwa yeyote atakaeyaona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PHQ/IRI/IRI/7043/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARY KOKUTEKELEZA RUGASHUMBA** anatangaza kupotea kwa akdi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 221 EFB,** CHASSIS NAMBA **ZRR700056013** na ENGINE NAMBA: **3ZR4069222.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/49412/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**REHEMA RASHID MWALIMU** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T164 BZU.** CHASSIS NO-**KZJ950042490** ENGINE NO- **KOKZJ95W** AINA YA GARI -LANDCRUSER PRADO.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI **PHQ/ARU/ARU/14942/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 21/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU CONSOLOTHA LONGINO WA ...................**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA DEVOTHA DAUDI MWAILUPE**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahkama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 mwezi 06 mwaka 2024

Zingatia;

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

Imetolewa leo tarehe 24 Mwezi 05 Mwaka 2024

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa D,SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 743 /2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SEIF ALLI MBONDE WA MTONI**

**KATIKA SHAURII LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SHABANI SEIF MBONDE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 mwezi 6 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo 23 Mwezi 5 Mwaka 2024.

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MOSHI SUB- REGISTRY**
**AT MOSHI**

**MISC.CIVIL APPLICATION NO.39 OF 2023**

**(C/F Talaka 14/2020, Moshi Urban Primary court and Matrimonial Appeal No. 06/2020**

**SAIDA RAJABU CHADUA............ .........APPLICANT**

**VERSUS**

**CHARLES JACOB NDAGULA ............RESPONDENT**

**TO: CHARLES JACOB NDAGULA.**

**NOTICE FOR MENTION,**

**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 25th June , at 9:00 a.m. before Honourable **L. M. MONGELLA,** judge.

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe .

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 22th day May,2024

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 10419 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late PETER AMOS MALEKELA of Dodoma City.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**SALAMA PETER MALEKELA AND OSCAR PETER MALEKELA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 21ST Day of JUNE, 2024

Dated at Dodoma this 23rd Day of May, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mataifa matano yafanya luteka ya kijeshi Niger

**NIAMEY,** NIGER

MATAIFA matano ya Kanda ya Sahel yanafanya luteka ya kijeshi magharibi mwa Niger, ikiwa ni mara ya kwanza kwa shughuli ya aina hiyo kufanywa katika eneo linalokumbwa na machafuko ya makundi ya itikadi kali.

Inaelezwa kuwa eneo la Sahel kwa miaka mingi limekuwa likikabiliwa na waasi wanaojihami kwa silaha wenye mfungamano na makundi ya Al-Qaeda na Dola ya Kiislamu.

Wizara ya Ulinzi ya Niger ilisema mataifa matano ambayo ni Burkina Faso, Mali, Chad, Niger na Togo tangu Jumatatu wiki iliyopita yamekuwa yakifanya mazoezi makubwa ya kitaifa katika kituo maalum cha mafunzo ya kijeshi mjini Tillia.

Ilieleza kuwa mazoezi hayo ni pamoja na mbinu za kivita na mipango inayolenga kuimarisha uhusiano kati ya jeshi na raia wa maeneo yanayokabiliwa na vita. Shughuli hiyo inayotarajiwa kukamilika Juni 3, mwaka huu inaashiria luteka ya kwanza ya kijeshi ya pamoja kati ya nchi hizo tano.

Awali tawala za kijeshi nchini Burkina Faso, Niger na Mali ziliwafukuza wanajeshi wa Ufaransa, mtawala wa zamani wa kikoloni, na zinaigeukia Russia kwa msaada.

Nchi hizo zilifikia mkataba wa ulinzi, unaofahamika kama Muungano wa Mataifa ya Sahel, na mwezi Februari zikatangaza kujiondoa katika Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS).

***DW***



Wafuasi wa Chama tawala Afrika Kusini cha African National Congress (ANC) wakiwa katika mkutano wa kuhitimisha kampeni za kisiasa juzi jijini Johanesburg. **PICHA: MTANDAO**

## Upinzani waomba Waafrika Kusini kuiangusha ANC

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

CHAMA kikuu cha upinzani Afrika Kusini Democratic Alliance (DA) kimetoa wito wake wa mwisho kwa wapigakura kukisaidia kukiondoa madarakani Chama Tawala cha African National Congress (ANC) wakati kikikamilisha kampeni zake kabla ya uchaguzi wa wiki hii.

Kauli hiyo imejiri baada ya vyama vikuu vinne vya kisiasa nchini Afrika Kusini, kuhitimisha kampeni zao kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Jumatano, wakati chama tawala ANC kikiwa njia panda.

Katika kile kilichotajwa kama kuonyesha kuwa bado kina ushawishi mkubwa katika siasa za nchi hiyo, chama tawala ANC kilikusanya umati mkubwa jana jijini Johanesburg, kikiahidi kuleta mabadiliko licha ya tuhuma za rushwa na shida au kupanda kwa gharama za maisha.

Akizungumza katika mkutano wa kuhitimisha kampeni ya kiongozi wa Democratic Alliance, John Steenhuisen, alitoa wito kwa wapigakura, kukipigia kura chama chake kwa sababu hakitoi ahadi tupu, siku chache kabla ya uchaguzi ambao unaweza kushuhudia chama tawala ANC kikipoteza wingi wake wa viti kwa mara ya kwanza.

Steenhuisen alisema kama wapigakura wa Democratic Alliance watabaki majumbani, au kuigawa kura miongozi mwa vyama vingi vidogo, basi sura ijayo ya nchi hiyo itakuwa mbaya hata zaidi kuliko siku za nyuma.

Democratic Alliance ndicho chama kikubwa kabisa nchini Afrika Kusini na kimekusanya baadhi ya vyama vidogo vya upinzani ili kuunda mkataba unaojulikana kama mkataba wa vyama vingi vya siasa nchini Afrika Kusini.

Aidha, ilielezwa kuwa muunganiko huo utavifanya vyama hivyo kuweka pamoja kura zao ili kukipinga chama tawala cha ANC baada ya uchaguzi. Huku uchunguzi wa maoni wa karibuni wachambuzi wakidokeza kuwa huenda ANC kikapata chini ya asilimia 50 ya kura za kitaifa.

Democratic Alliance wako chini ya shinikizo baada ya ungwaji mkono wao kupungua katika uchaguzi uliopita wa kitaifa na viongozi wake kadhaa wakaondoka chama hicho ili kuunda vyama vipya vya kisiasa ambavyo vitashiriki katika uchaguzi wa huo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa DA inayounga mkono biashara inaendesha serikali ya jimbo la Western Cape na makazi ya mji maarufu wa utalii wa Cape Town.

Ilielezwa kuwa kura za maoni zinabashiri ANC kupoteza wingi wake wa viti bungeni kwa mara ya kwanza, tangu Nelson Mandela alipopigiwa kura kuingia madarakani mwaka 1994 na kumaliza ubaguzi wa rangi.

Kwa upande wa chama cha upinzani cha The Economic Freedom Fighters (EFF) cha kwake Julius Malema, nacho kilihitimisha kampeni zake sambamba na ANC, ambako na chenyewe kiliahidi kufanya mabadiliko makubwa ya sera na ardhi na kufufua uchumi.

Vile vile, Chama cha Umkonto We Sizwe, kinachoongozwa na rais wa zamani Jacob Zuma, katika kuhitimisha kampeni zake, kimewataka raia kuiangusha serikali iliyoko madarakani, kikijinasibu kuwa na sera mbadala kuijenga nchi hiyo.

Kuhitimishwa kwa kampeni hizo za kisiasa nchini Afrika Kusini ni ishara kuwa maamuzi sasa yako mikononi mwa raia wa nchi hiyo, ambao watapiga kura Jumatano, kuamua mustakabali wao, katika moja ya uchaguzi unaotajwa utakuwa na upinzani mkali.

***RFI, DW, VOA***

# Shambulio la Israel laua 35 Rafah

**GAZA,** PALESTINA

WAPALESTINA 35 wakiwemo watoto na wanawake, wameuawa baada ya wanajeshi wa Israel kushambulia mji wa Rafah, licha ya Mahakama ya Kimataifa ya Haki (IAC), wiki iliyopita, kuagiza taifa hilo kusitisha operesheni kwenye mji huo na kuruhusu misaada ya kibinadamu kuwafikia wenye uhitaji.

Israel ilisema jana kwamba shambulizi katika ujirani wa Tel Al-Sultan huko Rafah, ambalo limemuua mkuu wa wafanyakazi wa Hamas kwa Ukingo wa Magharibi na ofisa mwingine mwandamizi, lilifanyika kwa kutumia silaha zenye shabaha ya uhakika.

Licha ya kauli hiyo Wizara ya Afya inayoendeshwa na Hamas huko Ukanda wa Gaza ilisema shambulizi limesababisha mahema kushika moto katika eneo ambalo linawahifadhi watu wasiokuwa na makazi.

Aidha, maofisa hao walibainishwa kuwa dazeni ya watu pia walijeruhiwa, huku Jamii ya Mwezi Mwekundu ya Palestina ikitarajia idadi ya vifo itaongezeka.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Israel lilikiri kutekeleza mashambulio ya anga, kuwalenga wapiganaji wa Hamas kwenye mji huo wa Rafah, unaopatikana, Kusini mwa Gaza na kwamba inafahamu kuwa kuna Wapalestina wa kawaida ambao wameuawa na kujeruhiwa.

Kupitia taarifa iliyotolewa na jeshi hilo lilisema, ndege yake ya kivita imevamia ngome ya Hamas, shambulio lililosababisha moto kuwaka pamoja na kusababisha madhara kwa wananchi wa kawaida.

Hata hivyo, kundi la Hamas lilisema, shambulio hilo, liliwalenga Wapalestina wanaoishi kwenye kambi ya wakimbizi inayosimamiwa na Umoja wa Mataifa (UN).

Wakati hayo yakijiri, Waziri Mkuu wa Israeli Benjamin Netanyahu, alisema hawezi kusitisha vita vya Gaza, wakati huu nchi tatu za Ulaya ikiwamo Ireland, Uhispania na Norway, zikitangaza kuwa tarehe 28 mwezi huu, zitatambua taifa la Palestina.

***RFI, VOA***

# Mbio za 'binti' zafana dar

**Na Faustine Feliciane**

MSIMU wa tatu wa mbio za ,Run for the binti' umefanyika mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya Oysterbay na kukutanisha zaidi ya wakimbiaji 700.

Mbio hizo ziliandaliwa kwa pamoja na taasisi ya huduma za kisheria ,Legal Services Facility, LSF' na ,Smile for Community (S4C) zikiwa na lengo la kuchangisha fedha na kusaidia watoto wa kike.

Akizungumza kabla ya kuanza mbio hizo, Waziri wa Katiba na Sheria, Pindi Chana kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, alisema serikali inatambua juhudi za mashirikia na taasisi zisizo za kiserikali katika kutatua changamoto kwa jamii.

„Niwapongeze LSF kwa kushirikiana na Smile for Community kwa kuandaa mbio hizi ambazo zimeweza kutuleta pamoja. Kama serikali, tunatambua na kuthamini juhudi zinazofanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kusaidia maendeleo ya jamii na kutatua changamoto zinazowakabili watoto wa kike hivyo tunaunga mkono jitihada hizi.

Aidha, alisema serikali imeanza kampeni maalumu inayowasisitiza wananchi kufanya mazoezi na kuwataka kutumia fursa hiyo kushirikiana kutimiza malengo ya kampeni hiyo.

Mbio hizo zilitoa elimu kwa watoto wa kike juu ya kupata elimu bora, elimu ya afya ya uzazi, utunzaji wa mazingira pamoja na kuimarisha afya kupitia mazoezi.

Aidha, Mkurugenzi wa Smile for Community, Flora Njelekela, alitoashukurani kwa mgeni rasmi kwa kuridhia na kuipa uzito mbio hizo ambapo watu walikimbia nusu marathoni (Kilometa 21), kilometa 10 na kilometa tano.

„Hii inaonesha wazi kuwa serikali inaunga mkono juhudi zinazofanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kutatua changamoto za kijamii," alisema Njelekela.

Pia alibainisha matokeo yanayotarajiwa baada ya mbio hizo. „Fedha zilizokusanywa leo zitaelekezwa moja kwa moja kwenye ujenzi na kuboresha miundombinu ya vyoo, kutoa majisafi kwa kujenga visima shuleni, kusambaza taulo za kike zinazoweza kutumika tena, kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi na matumizi sahihi ya nishati safi," alisema Njelekela.

Waziri wa Katiba na Sheria, Pindi Chana, akishiriki mbio za Run for Binti zilizofanyika Viwanja vya Oysterbay, ikiwa ni msimu wa tatu wa mafanikio wa mbio hizi zinazoratibiwa na kuandaliwa na Smile for Community (S4C) kwa kushirikiana na Legal Services Facility (LSF) jijini Dar es Salaam juzi. PICHA: MPIGAPICHA WETU



# MUHIMBILI, MUHAS WAJIPANGA AFCON

**Na Christina Mwakangale**



HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS), wamejipanga kwa ajili ya kutoa huduma za dharura wakati wa fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2027).

Fainali hizo za mwaka 2027 zimepangwa kufanyika kwa pamoja katika nchi tatu za Tanzania, Kenya na Uganda.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Muhimbili, Profesa Mohamed Janabi, akifafanua kuhusu suala hilo, jana, wakati wa uzinduzi Mwongozo wa Huduma za Dharura wa hospitali hiyo, alisema matarajio ni kutoa huduma zaidi za aina hiyo, kutokana na wingi wa watu watakaohudhuria mashindano.

Janabi, alisema MNH ilianza kujiandaa mapema kushiriki katika kutoa huduma, kwa kubainisha uwezo wake na vifaa, hivyo AFCON ikaridhia na yeye ni miongomi mwa wajumbe wa kamati ya maandalizi kwenye mashindano hayo.

"Muhimbili kwa siku tunaona wagonjwa wa dharura 150 hadi 200 na Mloganzila tunaona 30 hadi 35, katika hao aidha asilimia moja ya tuliowapokea kwa siku tutawapoteza au tusiwapoteze kabisa, kutokana na umahiri wa watoa huduma na vifaa.

"Mwaka jana na pekee, kwa hizi kampasi zetu mbili, tumeona takribani wagonjwa 21,000. Utaona umuhimu wa eneo la dharura. Wanaoongoza kuonwa hapa ni wagonjwa wa ajali, inapotokea ajali kitu cha kwanza ni kuzuia uvujaji damu," alisema Prof. Janabi.

Mwakilishi wa Makamu Mkuu wa chuo MUHAS, Dk. Doreen Kamori, alisema chuo hiho kimeongeza kozi na udahili wa wanafunzi wanaosoma kutoa huduma za dharura kutoka sita, mwaka 2010 hadi 25, mwaka huu.

"Huduma za dharura na uokoaji hutokea nje ya hospitali. Siku ya Kimataifa ya Huduma za Dharura huadhimishwa kila mwaka. Taifa tunajiandaa kuandaa mashindano makubwa, AFCON, kutakuwa na ongezeko la watu, tunazungumza na wadau kuimarisha huduma bobezi na dharura," alisema.

**SOKA**

## TWIGA STARS KUJIPIMA SUDAN KUSINI, MALI

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya taifa ya soka ya wanawake ,Twiga Stars' kinatarajia kucheza michezo miwili ya kirafiki dhidi ya Sudan Kusini na Mali, mwishoni mwa mwezi huu ikiwa sehemu ya maandalizi ya Fainali za Mataifa ya Afrika zitakazofanyika nchini Morocco.

Twiga Stars wanaendelea kufanya mazoezi yao katika kituo cha ufundi cha Shirikisho la Mpira wa miguu Tanzania (TFF) kilichopo Kigamboni.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema wiki hii Tanzania itapokea timu kutoka mataifa matatu kwa ajili ya michezo ya kirafiki kwa wanawake.

Alitaja mataifa hayo ni Mali, Sudan Kusini na Shelisheli ambapo michezo hiyo itachezwa kati ya Mei 29 na 31 mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

"Kila timu itapata nafasi ya kucheza mechi mbili ambazo ni kwa ajili ya kujiandaa na mashindano yaliyopo mbele yao, mataifa haya ni makubwa sana na inaonyesha jinsi gani soka la wanawake linavyozidi kukua.

Kuhusu timu ngeni tayari zimewasili na waamuzi watakaochezesha mechi hizo watakuwa Watanzania, hii ni kuendeleza soka la wanawake ili lizidi kukua," alisema Ndimbo.

Aliongeza kuwa tayari wachezaji wote wanaocheza soka la kulipwa nje ya Tanzania wameanza kuwasili na wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya michezo hiyo miwili ya kirafiki.

## ZISIKUPITE

### MCKENNA KUSUBIRI MAN
KOCHA wa Ipswich Town, Kieran McKenna, ambaye amekuwa akihusishwa na klabu za Brighton na Chelsea, atasubiri ofa kutoka katika klabu yake ya zamani ya Manchester United, ambako aliwahi kufanya kazi kama mkufunzi.***(Time)***

### POCHETTINO KUBAKI EPL
MAURICIO Pochettino angependa kusalia katika Ligi ya England baada ya kuondoka Chelsea na huenda akavutiwa na kazi ya kuinoa Manchester United ikiwa wataachana na Erik Ten Hag. ***(Standard)***

### CHELSEA YASAKA KOCHA
CHELSEA inatarajiwa kufanya mazungumzo na Kocha wa Leicester City, Enzo Maresca wakati wakiendelea na harakati zao za kutafuta mrithi wa Mauricio Pochettino. ***(Standard)***

### ENZO KIPENGELE
KIPENGELE cha kuachiliwa kwa Enzo Maresca katika mkataba wake na Leicester kinaaminika kuwa takribani pauni milioni 7.5. ***(Talksport)***

### ZEBRI NA CHELSEA
CHELSEA haijaondoa uwezekano wa kumnunua Roberto de Zerbi, ambaye aliondoka Brighton kwa makubaliano mwishoni mwa msimu huu. ***(Telegraph)***

### SANCHO KUJADILIWA
KLABU ya Borussia Dortmund inatarajiwa kufanya mazungumzo kuhusu kubadilisha mkataba wa mkopo wa winga wa Manchester United, Jadon Sancho kuwa wa kudumu baada ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini uwezekano wa kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 hauonekani kutokana na bei kubwa ya kumnunua. ***(Sky Sports)***

### KOMPANY NA BAYERN
KLABU ya Bayern Munich itampa kocha wa Burnley, Vincent Kompany mkataba hadi 2027 ili kuwa kocha wao mpya, huku klabu hiyo ya Ujerumani wakiwa katika awamu ya mwisho ya mazungumzo kuhusu kumwajiri Mbelgiji huyo. (Sky Sports)

### GASPERINI KUSAINI TENA
GIAN Piero Gasperini anakaribia kusaini mkataba mpya na Atalanta baada ya kushinda Ligi ya Europa. ***(L'Eco)***

### KLABU ZA SAUDIA KUSUBIRI
KLABU za Saudi Arabia ziko tayari kusubiri hadi msimu ujao kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Liverpool kutoka Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31 na kiungo wa kati wa Manchester City na Ubelgiji Kevin de Bruyne mwenye miaka 32, kwa uhamisho wa bure ikiwa hawatawapata wawili hao msimu huu. ***(Telegraph)***

### COADY AWANIWA STOKE
KLABU ya Stoke City imeonesha nia ya kutaka kumsajili beki, Conor Coady mwenye miaka 31 kutoka Leicester ***(Teamtalk),***

### KONATE AGOMBEWA
KLABU ya Leicester City inajiandaa kushindana na klabu za Ufaransa Lyon na Brest kumnunua fowadi wa Burkina Faso, Mohamed Konate mwenye miaka 26 ambaye mkataba wake na klabu ya Urusi ya Akhmat Grozny unamalizika msimu huu. ***(Football Insider)***

## DONDO SOKA MA LAYA




# ARSENAL YAMNYATIA KIPA JUSTIN BIJLOW

**Wataka kumfanya mbadala wa golikipa Ramsdale anayetarajiwa kuondoka klabuni hapo na kujiunga na...**

**LONDON,** ENGLAND

ARSENAL inafikiria kumsajili mlinda mlango wa Feyenoord, Justin Bijlow wakitaka kumfanya mbadala wa Aaron Ramsdale, ripoti imedai.

Akiwa amepoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza kwa David Raya, ambaye mkopo wake kutoka Brentford utafanywa kuwa wa kudumu hivi karibuni, Ramsdale anatarajiwa kufikiria chaguo lake msimu huu wa majira ya joto na hivi karibuni alihusishwa na Newcastle United.

Huku Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akitamani kuwabakisha makipa wawili wa kiwango cha juu kwenye kikosi chake, gazeti la The Telegraph limesema kuwa mlinda mlango wa Feyenoord, Bijlow yupo kwenye rada.

Bijlow mwenye miaka 26, aliingia katika akademi ya vijana ya Feyenoord na kucheza mechi 93.

Liverpool pia wanasemekana kumfuatilia Bijlow na bei maalum ya kipa huyo haijatajwa.

Kelleher, Ramsdale na Bijlow wote wanakaribia kumaliza miaka miwili ya mwisho ya mikataba yao.

# MBAPPE: NITATANGAZA RASMI WAPI NAENDA

**MADRID,** HISPANIA

KYLIAN Mbappé amesema atatangaza wapi anakwenda msimu ujao „siku chache" zijazo baada ya kushinda Kombe la Ufaransa akiwa na PSG.

Mbappé anatarajiwa sana kujiunga na Real Madrid akiwa tayari amethibitisha kuwa ataondoka PSG mkataba wake utakapokamilika msimu huu wa majira ya joto.

Baada ya timu yake kushinda 2-1 dhidi ya Lyon kwenye mchezo wa fainali, Mbappé aliulizwa na waandishi wa habari kwa nini bado hajaweka wazi klabu yake ijayo.

"Kwa sababu nadhani jambo bora zaidi kufanya ni kumaliza kusema kwaheri," nahodha huyo wa Ufaransa alisema.

"Nilichotaka ni kumaliza vizuri. Kuna wakati wa kila kitu. Nitatangaza klabu yangu mpya kwa wakati muafaka. Zitakuwa zimebaki siku chache kwa hiyo hakuna tatizo."

Akishinikizwa na waandishi wa habari ikiwa hiyo inamaanisha kuwa uhamisho huo ungekuwa rasmi kabla ya timu ya taifa kukutana kujiandaa na michuano ya Ulaya, Mbappé aliongeza: „Bado sijui, bado kuna maelezo. Jambo muhimu zaidi lilikuwa kushinda na kupata uzoefu, hisia hizi za mwisho."

Mbappé alizungumza kuhusu kile alichohisi kucheza mechi yake ya mwisho PSG baada ya misimu saba.

"Nilikuwa na bahati ya kuipitia. Nilichokuwa nacho, nisingepitia mahali pengine popote. Sasa nitapata uzoefu wa kitu kingine na sehemu nyingine," alisema Mbappe.




## Xavi amwonya kocha mpya Barca

**BARCELONA,** HISPANIA

BAADA ya kumaliza muda wake kama kocha wa Barcelona kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Sevilla Jumapili, Xavi Hernández alisema anaamini kazi yake haijathaminiwa na kwamba mbadala wake atakuwa na kazi ngumu mikononi mwake.

Mabao ya Robert Lewandowski na Fermín López yaliwahakikishia Barca ushindi huo huku wakimaliza kampeni ya LaLiga wakiwa na pointi tatu siku mbili tu baada ya klabu hiyo kutangaza kwamba Xavi atafukuzwa mwishoni mwa msimu huu.

„Sidhani kazi tuliyofanya imethaminiwa vya kutosha ukizingatia hali mbaya tuliyofikia," alisema Xavi akiiambia DAZN baada ya kuifunga Sevilla.

„Barca walikuwa wa tisa kwenye msimamo tulipowasili mwishoni mwa 2021. Tulimaliza wa pili. Kisha, katika msimu mzima wa kwanza tukashinda mataji mawili LaLiga na Supercopa ya Hispania.

„Mwaka huu hatujawa katika kiwango kinachohitajika, lakini imekuja kwa undani katika michezo kadhaa muhimu. Ni aibu. Nina huzuni, lakini hii ni kazi ya kocha."

ESPN imefichua kuwa Hansi Flick atachukua nafasi ya Xavi, huku uteuzi wa kocha huyo wa Ujerumani ukitarajiwa kutangazwa siku zijazo.

„Lazima wajue ni hali ngumu, kwa sababu Barcelona ni klabu ngumu, lakini kwa sababu ya hali mbaya ya kifedha, juu ya sheria zote za utendakazi wa kifedha wa LaLiga," Xavi alisema alipoulizwa kama alikuwa na ushauri wowote kwa mrithi wake.

„Haitakuwa rahisi hata kidogo. Watateseka na watahitaji uvumilivu kwa sababu ni kazi ngumu sana. Kitu pekee ambacho kinaweza kuwaokoa ni kushinda, iwe wamewahi kuwa sehemu ya klabu au la.

„Nimetazamwa kupitia kioo cha kukuza na kiwango fulani cha matarajio kilitolewa, kwa sababu nilikuwa sehemu ya enzi bora zaidi ya Barca."

Awali Xavi alitangaza Januari kwamba angejiuzulu msimu huu wa majira ya joto, lakini alibatilisha uamuzi wake Aprili kabla ya kutimuliwa katika mkutano na rais wa klabu Joan Laporta Ijumaa.



## Rodri atakiwa kumrithi Kroos

**MADRID,** HISPANIA

HUKU Toni Kroos akipanga kustaafu kiangazi hiki, Real Madrid wana jicho moja kwa kiungo wa Manchester City, Rodri ili kuziba pengo la kiungo huyo Mjerumani, ripoti imedai.

Siku ya Jumanne, Kroos alitangaza uamuzi wake wa kutundika daruga baada ya Euro 2024, kuashiria mwisho wa muongo mzima wa kukaa na Los Blancos. Kuondoka kwake bila shaka kutaonekana Bernabeu, na Bodi ya Madrid lazima ichukue hatua haraka kupata mbadala wake. Kroos amekuwa kiungo katika safu ya kiungo ya Madrid kwa miaka mingi, akiamua kucheza kwa maono yake, safu ya pasi na akili ya kimbinu.

Mchezaji yeyote anayetarajiwa atahitaji sio tu kulingana na uwezo wa Kroos bali pia kuzoea mahitaji ya mtindo wa uchezaji wa Madrid na matarajio makubwa ya wafuasi wa klabu hiyo.

Kulingana na AS, ndoto inayolengwa na Madrid ni Rodri.

Akiwa bado ana mkataba wa miaka mitatu zaidi, Rodri hawezi kuuzwa katika klabu na Madrid wanafahamu vyema kwamba watahitaji shabaha nyingine msimu huu wa joto.

Kutokana na hali hiyo, viongozi wa Madrid wanaripotiwa kumwangalia Joshua Kimmich wa Bayern Munich.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 anaingia katika miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na anakaribia njia panda katika maisha yake ya soka.

Licha ya mkataba wake kuisha, Bayern wanatarajiwa kudai zaidi ya euro milioni 60 ili kuachana na Kimmich.

HABARI MICHEZO

# BIASHARA UNITED YAINGIZA MGUU MMOJA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Biashara United sasa italazimika kusaka matokeo ya jumla kwenye michezo yake miwili dhidi ya itakayotoka Ligi Kuu kucheza ‚Play Off' ili kupanda daraja.

Biashara juzi ilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mbeya Kwanza kwenye mchezo wa pili wa mchujo kuwania kupanda daraja msimu ujao na kucheza Ligi Kuu.

Ikicheza ugenini, Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara ambako Mbeya Kwanza inautumia kama uwanja wake wa nyumbani, Biashara United ilipata mabao yake mawili kupitia kwa Herbert Lukindo na Abeid Athumani.

Ilikuwa ni mechi ya mkondo wa pili, baada ya awali kushinda pia mabao 2-0 nyumbani, Uwanja wa Karume, Musoma, mkoani Mara, mchezo uliochezwa Mei 19, wafungaji wakiwa ni Abeid na Boban Zirintusa, hivyo kufanikiwa kupita kwenye hatua hiyo ya mchujo kwa jumla ya mabao 4-0.

Timu hiyo iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu wa 2021/22, sasa itasubiri mshindi kati timu zitakazomaliza nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu.

Timu hizo za Ligi Kuu zitacheza mechi ya mchujo ambapo mshindi wa jumla atabaki, na itakayofungwa itakwenda kucheza mechi ya ‚play off' na Biashara United.

Biashara na Mbeya Kwanza, zililazimika kucheza mchujo, baada ya kumaliza nafasi ya tatu na ya nne katika Ligi ya Championship.

Mbeya Kwanza ilimaliza nafasi ya tatu na pointi zake 65, Biashara United ikiwa ya nne, ilikusanya pointi 62 huku ikiziacha timu za KenGold na Pamba zikipanda Ligi Kuu moja kwa moja.

Msimu uliopita, Mashujaa FC, ilipanda Ligi Kuu kwa kushinda mechi yake ya ‚Play off' dhidi ya Mbeya City ambayo ililazimika kucheza mchezo huo baada ya kufungwa na KMC katika michezo miwili ya mchujo, nyumbani na ugenini.




Wachezaji wa Kagera Sugar FC (U20) wakijipongeza baada ya timu hiyo kutwaa ubingwa wa Ligi ya Vijana kwa msimu wa 2023/2024. Hafla ya kukabidhi kombe la ubingwa huo ilifanyika jana katika Uwanja wa Chamazi Complex, Dar es Salaam baada ya mchezo dhidi ya Dodoma FC na kuibuka na ushindi wa mabao 3-2. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tembo Warriors watoka patupu Misri

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya mpira wa miguu kwa watu wenye Ulemavu Tanzania 'Tembo Warriors' wameshindwa kufikia malengo ya kutafuta nafasi ya kufuzu ya kucheza Kombe la Dunia, 2026.

Tembo Warriors walishindwa kutafuta tiketi hiyo juzi baada ya kupoteza mechi ya kusaka nafasi ya saba katika michuano ya Afrika (AAFCON) kwa kukubali kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya wenyeji wa mashindano hayo Misri.

Kikosi hicho kinatarajia kurejea nchini Alhamisi Juni 30, baada ya fainali hizo za Afrika kumalizika jana.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salvatory Edward alisema vijana wake walipambana lakini haikuwa bahati kwao na sasa wanarejea kujipanga kwa msimu mwingine.

Alisema wanasikitika hawakufikia malengo ya kucheza fainali za Afrika na kushindwa kutafuta tiketi ya kuwa miongoni mwa timu saba zitakazoshiriki Kombe la Dunia.

"Tumepoteza vyote tunarejea nyumbani kujipanga kwa wakati mwingine, mashindano yalikuwa mazuri wachezaji walipambana na tunakiri kuna sehemu tulizidiwa.

Malengo yetu yalikuwa kucheza fainali za Afrika tukashindwa kwa kuondolewa robo fainali na tukawa na nafasi ya kutafuta mshindi wa saba ili tuweze kufuzu Kombe la Dunia lakini tumepoteza dhidi ya Misri," alisema kocha huyo.

## U-20 Kagera Sugar wakabidhiwa kombe

**Na Faustine Feliciane**

KIKOSI cha Timu ya Vijana ya Kagera Sugar (U-20) juzi walikabidhiwa rasmi kombe lao la ubingwa na mdhamini wa ligi hiyo Benki ya NBC baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kagera Sugar wamekabidhiwa kombe hilo baada ya kuibuka mabingwa wa ligi hiyo na kuzishinda timu nyingine 15 zilizokuwa zikishiriki ligi hiyo.

Kombe hilo la ubingwa walikabidhiwa na Mkurugenzi wa Hazina na Masoko ya Fedha wa Benki hiyo, Peter Nalitolela mbele ya Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Nalitolela alisema tukio hilo limehitimisha utoaji vikombe vya ligi zote tatu zinazodhaminiwa na benki hiyo kwa msimu 2023/2024 ambapo tayari walianza kukabidhi kikombe cha cha Ligi ya ‚Championship' kwa timu ya Kengold FC ya Mbeya mapema mwezi huu huku makabidhiano ya kikombe kingine yakiwa ni yale yaliyofanyika mwishoni mwa wiki ambapo ilishuhudiwa benki hiyo ikitumia helikopta kubeba kombe la Ligi Kuu Tanzania Bara na kulikabidhi kwa mabingwa, Yanga. "Kimsingi tunawapongeza sana vijana wa Kagera Sugar kwa mafanikio haya na hivyo wanaungana na mabingwa wengine wawili ambao tayari wamefanikiwa kutwaa ubingwa.'"

# Pazia Ligi Kuu Bara kufungwa

INATOKA UK. 24

Mashujaa FC watakuwa nyumbani ikiwakaribisha Dodoma Jiji FC. Lake Tanganyika, Kigoma na Ihefu FC dhidi ya Mtibwa Sugar ambaye tayari ameshuka daraja.

Katika michezo ya leo kuna kuwania nafasi ya pili lakini vita vikali ipo katika kuwania tuzo ya ufungaji bora kati ya viungo washambuliaji wawili Stephen Aziz Ki wa Yanga na Feisal Salum 'Fei Toto' wote wakiwa wamefunga mabao 18.

Lakini kuna timu ambazo zinajinasua kushuka na kutafuta nafasi ya kucheza Play Off ambapo Geita Gold FC ambao wako nafasi ya 15 ya pili kutoka chini anakutana na Azam FC ambayo nayo ipo katika vita vya kutafuta nafasi ya pili ili kwenda kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Matumaini ya Simba kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao yamebebwa na Geita Gold FC ambaye akimfunga Azam FC, anaenda kucheza Play Off na kuwapa nafasi timu ya Wekundu wa Msimbazi kwenda kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa.

Kuelekea mchezo huo Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema maandalizi ya mchezo wa leo upo vizuri na muhimu kwao kupata matokeo ya ushindi. "Naweza kesho (leo), ndio tunafunga shule kwa sababu tunamaliza mechi ya mwisho wa kumaliza ligi ni muhimu kwetu kushinda na kufikia malengo yetu, mechi hii ni ya maamuzi na kila mmoja ana mahitaji yake. Itakuwa mechi inayohitaji umakini na dakika 90 tutapata uamuzi.

Licha ya kufanya vizuri lakini wachezaji wangu wapo vizuri kisaikolojia na wanafahamu umuhimu wa kushinda mchezo wa leo," alisema Mgunda.

Kocha Msaidizi George Mketo alisema wamejiandaa kwa mchezo wa leo wanaimani utakuwa mchezo mgumu kulingana na mahitaji ya kila timu kwa upande wao kupata matokeo mazuri.

Alisema wafahamu ubora wa Simba hasa katika maeneo ya pembeni na kati kwa kuwa na nguvu na wanaenda kupambana kutafuta matokeo chanya na kupata alama.

"Simba ina wachezaji wakubwa na wakomavu na tunaenda kucheza kwa namna mbili kukabilian na ubora wa wapinzani wetu na kufanikiwa kuvuna alama muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusalia katika ligi," alisema Mketo.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi alisema wachezaji wako vizuri na wapo tayari kwa mchezo huo, wanacheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu ya ubora wa mpinzani wao.

Alisema hakuna siri yoyote zaidi ya wachezaji kupambana na mashabiki wao kuwaunga mkono katika kila hali na anaimani ya kufanya vizuri katika michezo miwili iliyosalia leo dhidi ya Tanzania Prisons na fainali ya Kombe la Shirikisho la CRBD Bank dhidi ya Azam FC. "Tumefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo wetu dhidi ya Tanzania Prisons, wachezaji wanatambua tunahitaji nini katika mchezo wetu wa leo, kuna baadhi ya nyota nitawakosa akiwamo Jonas Mkude," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Ahmad Ally, alisema wanafahamu wanakutana na timu bora. Wamefanikiwa kuwaona Yanga walipocheza na Tabora United kwa kuona ubora wao.

"Ili uwe bora lazima ukamfunge aliyekuwa bora, ninawaheshimu na kuwapa nafasi wao na kucheza mpira kwa umakini na kuwapa presha, tunajua uhitaji wa hii mechi na sasa ligi imekuwa mgumu hasa nani anayecheza play off.

Ukiangalia msimamo unaona hakuna mwenye uhakika wa kubaki kwenye ligi kulingana na mtu anayeshika nafasi ya tano anaweza kuporomoka hadi chini asipokuwa makini katika mchezo huu wa leo, tunahitaji kupambana kutafuta matokeo mazuri," alisema Ahmad.

# Michezo

Jumanne Mei 28, 2024

Nipashe


## Arsenal yamnyatia Bijlow



UKURASA 21



CHAMA



AUCHO

# Aucho atamani kucheza na Chama

●●● Afunguka kukoshwa na uwezo wa mchezaji huyo na angependa...

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Yanga, Kharid Aucho ameweka wazi matamanio yake ya kuona siku moja anacheza timu moja na kiungo wa Simba raia wa Zambia, Clatous Chama.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Aucho, alisema anavutiwa sana na uwezo wa Chama na angetamani kucheza naye kwenye timu moja.

Alisema mchezaji huyo ana uwezo mkubwa na kipaji cha hali ya juu na anaweza kucheza kwenye timu yoyote.

„Chama anaurahisisha mpira, anafanya mpira uwe mwepesi, napenda namna anavyocheza... ndio mchezaji anayenivutia zaidi tangu nimekuja Tanzania," alisema Aucho.

Aidha, alisema kuwa atafurahi siku moja kumuona mchezaji huyo akiichezea Yanga na kucheza naye kwenye kikosi kimoja.

„Kama atakuja Yanga itakuwa vizuri zaidi, Chama anakufanya uone mpira wa miguu ni mchezo mwepesi, nimekuwa nikimwangalia akicheza, ikitokea kucheza naye itakuwa poa zaidi, kwangu ni mchezaji mzuri sana," alisema Aucho.

Kiungo huyo raia wa Uganda, alisema hayo ni maoni na matamanio yake binafsi kwa kuwa mchezaji huyo yupo kwenye timu nyingine lakini ni mmoja wa nyota anayemkubali kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

„Hata alipokwenda Morocco nilikuwa namfuatili na baadaye akarejea tena Tanzania, ana kipaji kwa kweli," alisema Aucho.

Chama, mkataba wake wa kuitumikia Simba unamalizika msimu huu na kwa sasa yupo kwenye mazungumzo na uongozi wa klabu hiyo kwa ajili ya kusaini mkataba mpya kuendelea kuwatumikia wekundu hao wa Msimbazi.

Hata hivyo, taarifa za ndani zinaeleza licha ya Yanga kumtaka Mzambia huyo, mwenyewe amekubali kusaini mkataba mwingine wa kuendelea kuitumikia Simba.

# Pazia Ligi Kuu Bara kufungwa leo

**Na Waandishi Wetu**

LIGI Kuu Tanzania Bara inafikia tamati leo kwa nyasi za viwanja nane kuwaka moto. licha ya kujulikana bingwa wa msimu huu lakini vita vikali vipo kutafuta mshindi wa pili katika ya Azam FC na Simba.

Michezo ya leo ni mabingwa wapya wa msimu huu Yanga, kukamilisha ratiba dhidi ya Tanzania Prisons, Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi. Simba watawakaribisha JKT Tanzania Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam.

Mechi zingine ni Geita Gold FC wakiwa nyumbani Uwanja wa Nyankumbu akimkaribisha Azam FC, Namungo FC dhidi ya Tabora United, Majaliwa Stadium, Lindi, Singida Fountain Gate FC dhidi ya Kagera Sugar Uwanja wa CCM Kirumba.

Coastal Union dhidi ya KMC FC, Uwanja wa Mkwakwani, Tanga,

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >